# KIKAO CHA 1

## INGIA

**(dakika 1)**

Waruhusu washiriki wote na mwezeshaji waingie.

Au zume.training/checkin na utumie msimbo: **5678**

## OMBA

**(Dakika 5)**

Anza na maombi. Ufahamu wa kiroho na mabadiliko hayawezekani bila Roho Mtakatifu. Chukua muda kama kikundi kumwalika Yeye ili akuongoze katika kipindi hiki.

## MAPITIO

**(dakika 1)**

**Katika somo hili, tutasikia na kujadili dhana hizi:**

- Mungu Anatumia Watu wa Kawaida
- Ufafanuzi Rahisi wa Mwanafunzi na Kanisa
- Kupumua Kiroho

**Na tutaongeza zana hizi kwenye seti yetu ya zana:**

- S.O.A.P.S. Kusoma Bibilia
- Makundi ya Uwajibikaji

## SOMA

**(Dakika 5)**

**Mungu Anatumia Watu wa Kawaida**

Karibu kwenye mafundisho ya Zúme. Zúme ni neno la Kigiriki linalomaanisha “chachu.”

Yesu anatuambia kwamba Ufalme wa Mungu ni kama mwanamke ambaye alichukua kiasi kidogo cha “ Zúme” na kukiweka kwenye kiasi kikubwa cha unga uliokandwa.

Alipokuwa akichanganya, chachu ilienea hata unga wote ukachachuka.

Yesu alikuwa anatufundisha kwamba mtu wa kawaida anaweza kutumia kitu kidogo sana na kusababisha kishindo kikubwa sana!

Ndoto yetu ni kufanya yale Yesu alisema -- kuwasaidia watu wa kawaida duniani kote kutumia vifaa vidogo kutoa vishindo vikubwa katika Ufalme wa Mungu!

Maagizo ya Yesu ya mwisho kwa wanafunzi wake yalikuwa rahisi. Alisema -- Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi – enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwa batiza kwa jina la baba, na la Mwana, nala Roho Mtakatifu, na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.

Maagizo ya Yesu yalikuwa rahisi –Mkawafanye Wanafunzi

Amri yake jinsi ya kutekeleza hayo ilikuwa rahisi – mkafanye wanafunzi popote muendapo

- Mkafanye wanafunzi kwa kuwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana na la Roho Mtakatifu
- Mkawafanye wanafunzi kwa kuwafundisha yote niliyowaamuru

Kwa hivyo ni hatua zipi za kuwafanya wanafunzi?

- Tunawafanya wanafunzi kila wakati – popote tuendapo na tunapoenda
- Mtu akifanya uamuzi wa kumfuata Yesu – sharti abatizwe
- Wanapokua – tufundishe kila mwanafunzi jinsi ya kutii vitu vyote alivyoamuru Yesu.

Kwa vile kitu kimoja alichoamuru ni kufanya wanafunzi, hiyo inamaanisha kila mwanafunzi anayemfuata Yesu anastahili kujifunza jinsi ya kutengeneza wanafunzi pia.

Hao wanafunzi wanastahili kutengeneza wanafunzi. Na hao wanafunzi nao wakatengeneze wanafunzi, pia.

Kuzidisha wanafunzi. Hivyo ndivyo  Zúme inafanya kazi.

Ni kama chachu – ilijichanganya ndani mwa unga uliokandwa hadi wote ukawa chachu.

Wakati Yesu alipotoa amri hii ya kwenda kuwafanya wanafunzi, alitoa ahadi pia.

Yesu alisema – Nitakuwa nanyi daima. Hata ukamilifu wa dahari.

Kila mfuasi wa Yesu anapaswa kuzingatia ahadi ya kuwa Yesu yu pamoja nasi. Kwa sababu Yeye yuko!

Lakini pia inamaanisha kila mfuasi wa Yesu anapaswa kujitoa kwa ukweli kwamba Yesu anataka kila mmoja wetu atengeneneze wanafunzi. Kwa sababu Yeye alifanya.

Yesu alisema – nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi enendeni mkawafanye wanafunzi.

Mamlaka ambayo Yesu hutegemea wakati Anatutuma - ni mamlaka Yake

Yesu anasema hakuna mamlaka iliyo juu kuliko hiyo. Hakuna utamaduni uliyo na mamlaka zaidi.

Hakuna utamaduni uliyo na mamlaka zaidi. Hakuna sheria duniani iliyo na mamlaka zaidi.

Yesu alisema – nendeni mkawafanye wanafunzi.

Na kama Zúme - chachu – tutaendelea kuenda na kukua hata kazi yote ikamilike.

## JADILI

**(dakika 10)**

Ikiwa Yesu alikusudia kila mmoja wa wafuasi Wake kutii Agizo Lake Kuu, kwa nini ni wachache sana wanaofanya wanafunzi?

---

## SOMA

**(Dakika 5)**

**Wanafunzi na Kanisa**

Karibuni tena kwenye mafundisho ya Zumé.

Katika kipindi hiki, tutazungumzia kuhusu wanafunzi na kanisa.

Mwanafunzi ni nani?

**Na wawezaje kumfanya mmoja? awe mwanafunzi kwa njia gani?**

Je, wawezaje kumfundisha mfuasi wa Yesu kutii amri zake zote?

Je, unachukuliaje mtu ambaye aliishi maisha yake kama mtumwa wa ulimwengu na kumwezesha kuwa raia wa ufalme wa Mungu?

Maana ya neno mwanafunzi ni mfuasi.

Kwa hivyo mwanafunzi ni mfuasi wa Mungu.

Yesu alisema – Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani.

Kwa hivyo katika ufalme wa Mungu, Yesu ndiye Mfalme wetu.

Sisi ni raia wake, kwa mapenzi yake.
Wapenzi wake, makusudi, malengo yake, vipaumbele na maadili ni vya juu na bora zaidi.

Neno lake ni sheria. Kwa hivyo sheria ya ufalme ni nini? Je! Yesu anawaambia watu wake wakafanye nini?

Yesu alisema - Mpende Bwana Mungu kwa moyo wako wote, kwa nafsi yako yote, kwa akili yako yote na kwa nguvu zako zote.
Yesu alisema - Mpende jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe.

Yesu alisema kwamba amri za Mungu ktika Agano la Kale - sheria zote na manabii - zinaweza kufupishwa katika mambo haya mawili - mpende Mungu na Uwapende Watu

Yesu alisema - Fanya wanafunzi

Yesu alisema - Wafundishe kutii yote niliyoamuru.

Kwa kuwa kufanya wanafunzi inajumuisha kuwafundisha yote Yesu aliyoamuru - Agano Jipya inaweza kufupishwa kwa jambo moja - Wafanye Wanafunzi

Mwanafunzi ni mfuasi wa Yesu anayempenda Mungu, anapenda watu na huwafanya wanafunzi

**Basi kanisa ni nini?**

Huenda huwa unafikiria kanisa ni jengo - mahali unapoenda.

Lakini Neno la Mungu linazungumzia kanisa kama mkusanyiko - watu ambao wewe umo miongoni mwao.

Neno "kanisa" linatumiwa katika Biblia kwa njia tatu tofauti:

- **kanisa la ulimwengu wote** – watu wote ambao walikuwa, ambao wapo na ambao daima watakuwa wafuasi wa Yesu
- **kanisa la jiji au la kanda** – watu wote wanaomfuata Yesu na wanaishi humo au karibu na eneo fulani la ulimwengu
- **kanisa la nyumbani** – watu wote wanaomfuata Yesu na hukutana pahali mmoja ama watu wengi wanapoishi.

Familia ya kiroho – wafuasi wa Yesu wanaompenda Mungu, wanawapenda watu na kuwafanya wanafunzi ambao hukutana kwenye mitaa yao ndio aina ya mwisho ya kikundi hiki cha kanisa – kanisa la nyumbani au kanisa vivi hivi.

Wakati makundi ya makanisa haya yanapokutana kufanya kitu kikubwa, kwapamoja, wanaweza kutengeza kanisa la jiji au kikanda.
Makanisa hayo yote vivi hivi yameunganishwa katika mikoa na kuenea katika historia kufanya kanisa zima.

HILO NI KANISA NA HERUFI "K" KUBWA
**Makanisa yakawaida ni familia za kiroho** na Yesu kama kiungo cha kati na mfalme wao.

Makanisa ya kawaida ni familia za kiroho za wanaompenda Mungu, wanawapenda wengine na wanawafanya wanafunzi ambao wanajizidisha.

Makanisa mengine yana majengo na orodha na matumizi na wafanyi kazi. Lakini makanisa yakawaida hayana haja na vitu hivi ili wampende Mungu, wapende wengine na kuwafanya wanafunzi ambao wanajizidisha idadi.

Na kwa kuwa chochote cha ziada hulifanya kanisa kuwa na ugumu kujizidisha, mafundisho yetu huacha vitu kama majengo na orodha na matumizi na wafanya kazikwa kanisa la jiji la kanda lililojengwa kutokana na uzidishaji wa makanisa yakawaida.

Kumbuka kwamba “zumé” inamaanisha “chachu” -- kiumbe ambacho kinazalisha haraka haraka.

Kupitia mafundisho ya Zumé – tutakuwa kama ile chachu – vivi hivi na kujizidisha.
Lakini kabla tuanze kujizidisha –tuhakikishe kwamba tunajua kile Mungu anataka kizalishwe.
Kwa sababu kuzidisha kunaweza kuwa kuzuri – lakini sio kila mara.

Saratani hujizidisha. Na inaua.

Tunawezaje kuzalisha uhai na sio kifo? Tunawezaje kuhakikisha kwamba sisi ni wanafunzi wanaoweza kuzalisha?

## JADILI

**(dakika 10)**

- Unapofikiria kuhusu kanisa, kitu gani huja mawazoni?
- Kuna tofauti gani kati ya picha hiyo na kile kinachofafanuliwa kwenye video kama "Kanisa Rahisi"?
- Unafikiri ni gani ingekuwa rahisi kuzidisha na kwa nini?

## SOMA

**(Dakika 5)**

**Kumsikia na Kumtii Mungu**

Karibu tena kwenye mafundisho ya Zumé.

Katika kipindi hiki, tutaongea kuhusu kusikia kutoka kwa Mungu na kutii yale tunayosikia.

Kupumua ni maisha.

Tunavuta hewa ndani. Tunatoa hewa nje, ni uhai.

Kupumua ni muhimu katika Ufalme wa Mungu.

Kwa kweli, Mungu anaita Roho Wake - "pumzi"

Katika Ufalme, tunapumua ndani tunaposikia kutoka kwa Mungu.

Tunapumua wakati tunasikia kutoka kwa Mungu kupitia NENO LAKE – Biblia.

Tunapumua wakati tunaposikia kutoka kwa Mungu kupitia kwa MAOMBI - mazungumzo yetu naye.

Tunapumua wakati tunasikia kutoka kwa Mungu kupitia MWILI WAKE - kanisa, wafuasi wengine wa Yesu.

Tunapumua tunaposikia kutoka kwa Mungu kwa njia ya kazi zake - matukio, uzoefu na wakati mwingine hata mateso na kuteseka ambapo anaruhusu watoto wake kupitia.

Katika Ufalme tunapumua NJE tunapotenda kwa ajili ya yale tunasikia kutoka kwa Mungu. Tunapumua NJE wakati TUNATII.

Wakati mwingine kupumua nje kwa KUTII inamaanisha kubadilisha mawazo yetu, maneno yetu au matendo yetu ili kuwaleta pamoja na Yesu na mapenzi Yake.

Wakati mwingine kupumua kwa KUTII kunamaanisha kugawana kile Yesu ameshiriki nasi - kupeana kile alichotupa - ili wengine waweze kubarikiwa kama vile Mungu anavyotubariki.

Kwa mfuasi wa Yesu - hii kupumua NDANI na kupumua NJE ni muhimu. Ni maisha yetu.

Yesu alisema - Mwana hawezi kufanya kitu peke yake. Anafanya tu yale anayoyaona Baba akifanya. Chochote Baba anachofanya, Mwana pia hufanya.

Yesu alisema – Sineni kwa mamlaka yangu mwenyewe. Baba aliyenituma ameniamrisha cha kusema na jinsi ya kusema.

Yesu alisema kwamba kila neno alilosema na kila kazi aliyotimiza ilitokana na KUSIKIA kutoka kwa Mungu na KUTII yale aliyasikia.

Pumua NDANI - Sikia kutoka kwa Mungu.

Pumua NJE - Tii yale unayosikia na ushiriki na wengine.

Yesu alisema kwamba wafuasi wake pia watasikia kutoka kwa Mungu kwa sababu ya Roho Mtakatifu wake - Kupumua Kwake - ambayo itapumuliwa ndani ya kila mmoja wetu anayemfuata.

Yesu alisema - Msaidizi, Roho Mtakatifu, ambaye Baba atamtuma kwa jina langu, atawafundisha vitu vyote na kuwakumbusheni kila kitu nilichowaambia.

Kupumua NDANI- Sikia kutoka kwa Mungu.

Pumua NJE- Tii yale unayoyasikia na uishiriki na wengine.

Yesu alikuwa anatuonyesha jinsi ya kuishi.

Kwa hivyo tunaisikiaje sauti ya Mungu? Tunajuaje nini cha kutii?

Yesu alijiita mwenyewe "Mchungaji Mzuri". Yesu aliwaita wafuasi "kondoo"wake.

Yesu akasema - Kondoo wangu husikia sauti Yangu, na ninawajua, na wananifuata.

Yesu alisema - Yeyote aliye wa Mungu husikia kile ambacho Mungu anasema. Sababu hamsikii ni kwamba ninyi si wa Mungu.

Kama wafuasi wa Yesu, tunapaswa kujitolea kusikia sauti Yake.

- TUNASIKIA sauti yake kwa kuwa kimya.
- TUNASIKIA sauti yake kwa kumzingatia Yesu.
- TUNASIKIA sauti yake katika mawazo yetu, maono yetu, hisia zetu na dhana zetu.
- TUNASIKIA sauti yake tunapoandika na kuhakiki kile tunachosikia.

Si kila sauti, sio kila wazo, sio maono, hisia au dhana ni sauti ya Mungu.

Wakati mwingine ni sauti ya adui

Yesu alisema adui yetu ni mwongo na baba wa uongo. Yesu alisema adui yetu huja kuiba, kuua na kuharibu.

Lakini Mungu anasema kwamba TUTASIKIA kutoka kwake na tutajua ni Yeye wakati anapozungumza

Kwa kujizoeza na maombi, tunaweza kujua sauti ya Mungu vyema. Tunaweza kujifunza kujua kama tunachosikia ni kutoka kwa Mungu au sauti nyingine.

Hapa kuna njia ya kujaribu yale tunayosikia:

- Wakati Yesu anapoongea - sauti yake itakuwa thabiti Neno lake Lililoandikwa -
- Biblia - tayari imetueleza. Sauti yake haitakinzana na sauti ilioandikwa.

- Wakati Yesu anapoongea - sauti yake itaipa mioyo yetu hisia ya tumaini na amani. Sauti yake haitatuacha ama kutuvunja mioyo. Yesu hahukumu. Yesu hurekebisha kwa upendo.
- Sauti ya Yesu haitaelezea matendo ya mwili - uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu na uchawi, uadai, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi, mambo haya sio sauti ya Mungu.
- Wakati Yesu anapoongea - sauti yake itatuonyesha matunda ya Roho wa Mungu - upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi.

Wakati Yesu akisema - Sauti yake hutupa hisia za kujiamini badala ya wasiwasi. Tunapata ndani mwetu ujuzi na amani kwamba kile tunachosikia kinatoka kwa Mungu. Hatuwezi kusikia kila kitu mara moja. Tunaweza kusikia sehemu tu ya kile tunachohitajika kujua. Lakini kile tunasikia itakuwa imara - si ya kuhama hama au kujibadilisha.

Habari njema kwa kila mfuasi wa Yesu ni kwamba tunapopumua NDANI na KUSIKIA kutoka kwa Mungu na tunapopumua NJE na KUTII tunachosikia na kushirikiana na wengine tulichosikia - Mungu ataongea wazi wazi.

Pumzi yake itapumua kupitia sisi hata zaidi.

TUTASIKIA sauti yake wazi zaidi.

TUTAJUA sauti yake na sio nyingine.

TUTAONA kazi ndani yake duniani na kujiunga naye kufanya kazi pamoja

Tunapumua. Tunapumua nje. Uzima.

## JADILI

**(dakika 10)**

- Kwa nini ni muhimu kujifunza na kusikia na kutambua sauti ya Mungu?
- Je, kusikia na kumuitikia Bwana ni kama kupumua? Kwa nini au kwa nini sivyo?

## SOMA

**(Dakika 5)**

**S.O.A.P.S. Kusoma Bibilia**

Yesu alisema -- “mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana na Roho Mtakatifu na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru…”

Ikiwa kila mfuasi wa Yesu atatii amri hii, basi wanastahili kujua yale Yesu aliamurisha.

Amri Kuu na Agizo Kuu ni ufupisho wa yale Mungu angeliwaambia, lakini ikiwa mfuasi atakua kwa jinsi Mungu alivyomuumba awe, basi wanastahili kujua na kutii hata na zaidi.

SOAPS inamaanisha:

- **Maandiko**
- **Uchunguzi**
- **Matumizi**
- **Maombi na**
- **Kushirikiana**

Njia rahisi ya kujifunza na kukumbuka wenye utaratibu wa kufaa wa kusoma Biblia ambayo kila mfuasi wa Yesu anaweza kutumia.

Ebu tuangalie kila sehemu kwa kina.

Wakati unaposoma ama unasikiliza Biblia:

- **Maandiko**: Andika kifungu ama vifungu vilivyo vya maana kwako, leo.
- **Uchunguzi**: Andika tena kwa maneno yako mwenyewe vifungu hivyo ama jambo lenye maana kutoka kwa maandiko kukusaidia kuelewa maana.
- **Matumizi**:  Fikiria inamaanisha nini kutii amri hii, ama dhana katika maisha yako mwenyewe. Je, unaweza kufanya nini tofauti? Ziandike
- **Maombi**: Andika maombi yanayomueleza Mungu yale umeyasoma kutoka kwa neno lake na yale umeelewa kuhusu kutii amri zake na kutumia yale uliyojifunza.
- **Kushirikiana**: Muulize Mungu ni nani angependa ushirikiane naye yale uliyojifunza na jinsi unavyoitumia.

Na tuone jinsi SOAPS inavyofanya kazi:

- **Maandiko** – Biblia inasema  -- “Mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu,” asema Bwana.  “kwa maana mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi,  ndivyo njia zangu zi juu kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu.”  Isaya 55:8-9
- **Uchunguzi** – Kama mwanadamu, nina ukadiri kwa yale ninayojua na yale ninajua jinsi ya kufanya. Mungu hajakadiriwa kwa njia yoyote. Anaona na anajua vitu vyote. Anaweza chochote.
- **Matumizi** – Kwa vile Mungu anajua mambo yote na njia yake ni bora, nitakuwa na mafanikio mema maishani ikiwa nitamfuata yeye badala ya kutegemea njia zangu mwenyewe ya kufanya mambo.

- **Maombi** – Bwana, sijui jinsi ya kuishi maisha mema yanayokuridhisha na kusaidia wengine. Njia zangu hunielekeza kwa makosa. Mawazo yangu hunielekeza kwa kuumia, badala yake nufundishe njia zako na mawazo yako, tfadhali. Acha Roho wako Mtakatifu aniongoze ninapokufuata.
- **Kushirikiana** – Nitashirikiana vifungu hivi na matumizi yake kwa rafiki yangu, Stefano, ambaye anapitia wakati mgumu na anahitaji uamuzi wa mwelekeo  anaokumbana nao.

Masomo ya Biblia ya SOAPS. Ni kitu rahisi sana katika kitabu cha Zume

---

## SHUGHULI

**(dakika 30)**

**Fanya mazoezi ya S.O.A.P.S.**

- Work individually through the SOAPS Bible study pattern using Matthew 6:9-13. (20 min)
- Rudini pamoja na mshiriki S.O.A.P.S. katika vikundi vya watu wawili au watatu. (dakika 10)

**MAUDHUI:**

**Maandiko**

Andika mstari mmoja au zaidi ambayo ni ya maana sana kwako, leo.

**Uchunguzi**

Andika upya mistari hiyo au mambo muhimu kwa maneno yako mwenyewe ili kuelewa vyema.

**Utendaji**

Fikiria juu ya nini maana ya kutii amri hizi katika maisha yako mwenyewe.

**Maombi**

Andika maombi ukimwambia Mungu yale uliyojifunza na jinsi unavyopanga kutii.

**Kushikiri**

Muulize Mungu ambaye anataka ushiriki naye kuhusu yale uliyojifunza/kutumia.

**Hapa kuna mfano wa S.O.A.P.S. kazini:**

S - "Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu," asema Bwana. "Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu." Isaya 55:8-9

O – Kama binadamu, nina mipaka katika kile ninachojua na kile ninachojua kufanya. Mungu hana kikomo kwa njia yoyote. Anaona na anajua YOTE. Anaweza CHOCHOTE.

A - Kwa kuwa Mungu anajua kila kitu na njia zake ni bora zaidi, nitakuwa na mafanikio zaidi maishani ikiwa nitamfuata badala ya kutegemea njia yangu mwenyewe ya kufanya mambo.

P - Bwana, sijui jinsi ya kuishi maisha mazuri yanayokupendeza na kusaidia wengine. Njia zangu husababisha makosa. Mawazo yangu husababisha maumivu. Tafadhali nifundishe njia Zako na mawazo Yako, badala yake. Acha Roho wako Mtakatifu aniongoze ninapokufuata Wewe.

S – Nitashiriki mistari hii na matumizi haya na rafiki yangu, Steve, ambaye anapitia wakati mgumu na anahitaji mwelekeo wa maamuzi muhimu anayokabili.

## SOMA

**(Dakika 5)**

**Makundi ya Uwajibikaji**

Yesu alisema - “Kila aliyepewa mengi, mengi yatahitajika kutoka kwake; na aliyepewa kusimamia mengi kwake kuhitajika zaidi.”

Yesu alitoa hadithi nyingi za uwajibikaji na kutuelezea ukweli jinsi tutakavyohusika kwa kile tunachofanya na kusema.

Yesu anatuambia mambo haya, ili tuwe tayari baadaye. Na kwa sababu tutawajibika kwake siku moja, ni vyema kujizoesha kuwajibika kila mmoja kwa mwenzake.

Makundi ya uwajibikaji yanajumuisha watu wawili au watatu wa jinsia moja – wanaume kwa wanaume na wanawake kwa wanawake – ambao wanakutana mara moja kwa juma ili kujadiliana maswali yanayoonyesha maeneo ambapo mambo yanaenda sawa na maeneo mengine ambayo yanayohitaji marekebisho.

Kila mfuasi wa Yesu atachukuliwa kama anayewajibika, kwa hivyo kila mfuasi wa Yesu anapaswa kujizoesha kuwajibikia wengine.

Makundi ya uwajibikaji. Chombo kingine rahisi katika kitabu cha zume.

## SHUGHULI

**(Dakika 20)**

**Mazoezi - Vikundi vya uwajibikaji**

- Mjigawanye kwa vikundi vya watu wawili au watatu wa jinsi moja.
- Tumia dakika 20 zinazofuata kufanya kazi pamoja kupitia Maswali ya Uwajibikaji.

**Maudhui:**

1. Umemuonaje Mungu akifanya kazi?
2. Je, umekuwa ushuhuda wiki hii kwa ukuu wa Yesu Kristo kwa maneno na matendo yako yote?
3. Je, umekabiliwa na nyenzo zinazovutia ngono au kuruhusu akili yako kuwaza mawazo yasiyofaa ya ngono?
4. Je, umekubali umiliki wa Mungu katika matumizi yako ya pesa?
5. Umetamani chochote?
6. Je, umeumiza sifa au hisia za mtu kwa maneno yako?
7. Je, umekuwa si mwaminifu kwa maneno au matendo au kutia chumvi?
8. Je, umejihusisha na tabia ya uraibu (au mvivu au isiyo na nidhamu)?
9. Je, umekuwa mtumwa wa mavazi, marafiki, kazi, au mali?
10. Umeshindwa kumsamehe mtu?
11. Je, ni wasiwasi gani au wasiwasi gani unaokumbana nao?
12. Je, umelalamika au kunung'unika?
13. Je, umedumisha moyo wa shukrani?
14. Je, umekuwa ukiheshimu, kuelewa na kuwa mkarimu katika mahusiano yako muhimu?
15. Je, ni majaribu gani katika mawazo, neno, au matendo ambayo umekumbana nayo na ulijibu vipi?
16. Je, umechukuaje fursa za kuwatumikia au kuwabariki wengine, hasa waumini?
17. Je, umeona majibu mahususi kwa maombi?

## ANGALIA

**(dakika 1)**

**Dhana zilizosikika katika kikao hiki:**

- Mungu Anatumia Watu wa Kawaida
- Ufafanuzi Rahisi wa Mwanafunzi na Kanisa
- Kupumua Kiroho

**Zana zilizosikika katika kikao hiki:**

- S.O.A.P.S. Kusoma Bibilia
- Makundi ya Uwajibikaji

---

**HATUA IFUATAYO**

## TII

Anza kufanya mazoezi ya S.O.A.P.S. Kusoma Biblia kati ya sasa na mkutano wako ujao. Zingatia Mathayo 5-7, soma angalau mara moja kwa siku. Weka jarida la kila siku kwa kutumia S.O.A.P.S. muundo.

## SHIRIKISHA

Tafuta mshirika wa uwajibikaji (jinsia sawa) na uanze kukutana naye kila wiki.

ZÚME

KIKAO CHA 2

## INGIA

**(dakika 1)**

Waruhusu washiriki wote na mwezeshaji waingie.

Au zume.training/checkin na utumie msimbo: **2468**

## OMBA

**(Dakika 5)**

Uliza kama kuna yeyote katika kikundi ana mahitaji maalum ambayo angependa kundi liombee.

Asante Mungu kwamba anaahidi katika Neno lake kusikiliza na kutenda wakati watu wake wanaomba.

Omba Roho Mtakatifu wa Mungu aongoze wakati wako pamoja.

## ANGALIA

Kabla ya kuanza, chukua muda kutazama nyuma.

## NYUMA

**(Dakika 5)**

Mwishoni mwa kipindi kilichopita, kila mtu katika kikundi chako alipewa changamoto ya kufanya mazoezi uliyojifunza.

Chukua muda mfupi kuona jinsi kundi lako lilivyofanya juma hili.

## MAPITIO

**(dakika 1)**

**Katika kikao hiki, tutasikia na kujadili dhana hii:**

- Mtayarishaji Sio Mtumiaji

**Na tutaongeza zana hizi kwenye seti yetu ya zana:**

- Mfuatano wa Maombi
- Orodha ya 100

## SOMA

**(Dakika 5)**

**Mtayarishaji Sio Mtumiaji**

Katika kikao hiki, tutazungumzia kuhusu jinsi tunaweza kumsaidia mfuasi wa Yesu kuwa MZALISHAJI katika ufalme wa Mungu badala ya mlaji tu. Katika mpango wake mkamilifu, Mungu alituumba tuishi katika usawa – KUZAANA na KULA, KUFANYIZA na KUTUMIA, KUMWAGA NJE na KUJAZWA ili tuweze KUMWAGA NJE tena.

Lakini, katika dunia yetu hii, watu wamekataa mpango wake Mungu, na wengi wanatumia nguvu zao kuishi nje ya sehemu ya ulinganisho wa Mungu.

WANAJIFUNZA bali hawashirikiani. WAMEJAZWA bali hawamwagi nje. WANATUMIA bali hawazilishi.

Ikiwa tutawafanya wanafunzi wanaojizidisha, basi tunahitaji kushiriki pamoja nao jinsi wanaweza kuwa wazalishaji na sio watumiaji tu.

Tunaweza kufanya hivyo hapa – Mungu anatumia Neno lililoandikwa – ambalo tunaita maandiko ama Biblia – ili kukua kiroho.

Kila mwanafunzi anahitaji kujiandaa ili akasome, kutafsiri na kutumia maandiko.

Zaidi ya maelfu ya miaka na kwa mikono ya waandishi wengi tofauti, Mungu alinena neno lake ndani  ya mioyo ya watu waaminifu ambao walishika na kushirikiana yale waliyoyasikia.

Maandiko yanatufundisha hadithi ya Mungu, mipango yake, moyo wake, njia zake.

Katika kikao cha awali, mlijifunza kuhusu vyombo viwili – masomo ya Biblia ya SOAPS na Kikundi cha Uwajibikaji. Katika kikao kijacho, mtajifunza chombo kimoja kingine – vikundi vya theluthi 3/3.

Vifaa hivi vitatu vinafanya kazi kwa pamoja ili kusaidia wafuasi wapya kujifunza, kutafsiri na kutumia Neno la Mungu lililoandikwa.

Watajifunza sio kuwa tu wasikizaji wa Neno la Mungu bali watendaji na washirika, pia.

Mungu hutumia Neno lake Lililonenwa – ambalo unaweza kutambua kwa njia ya maombi – kutufanya tukue kiroho.

Maombi ni kuzungumza na kumsikiliza Mungu. Maombi hutusaidia kumjua Mungu kwa ukaribu sana na kuelewa moyo wake, mapenzi yake na njia zake.

Maombi hutusaidia katika huduma na kuwatumikia wengine, hutusaidia kufundisha na kushiriki katika njia maalum ambayo husaidia mtu au kikundi kumjua Mungu vizuri.

Vifaa viwili - Kuomba kwa kutembea na kuomba kwa mviringo huwasaidia Wafuasi kuendeleza maombi ya kibinafsi na kujifunza maisha ya maombi ya kibinafsi na kuomba kwa njia ambazo zinahudumia wengine.

Vifaa hivi husaidia kuendeleza tabia ya kuomba bila kukoma na kujifunza kuona dunia kutokana na mtazamo wa kiroho badala ya kutegemea yale tunayoweza kuona tu.

Ikitumika kwa uthabiti, vinasaidia mfuasi wa Yesu, kuongeza uwezo wao wa maombi na kuongeza uwezo wao wa kusikia kutoka kwa Mungu na kushirikiana yale wanayoyasikia.

Mungu hutumia waumini Mwili wake – ambao tunaita Kanisa ama Wafuasi wa Yesu – kutukuza kiroho.

Kama mkusanyiko wa waumini, tumeunganishwa. Neno la Mungu linasema kwamba, katika Yesu – sisi ni sehemu nyingi za mwili mmoja, na tunahusiana. Kwa maneno mengine, hatujaunganishwa tu na Mungu – tumeunganishwa na kila mmoja.

Mungu anasema mjiwasilishe kila mmoja kwa mwenzake. Mungu anasema mkahudumiane.

Kila mmoja wetu ana uwezo tofauti na kila mmoja ana udhaifu. Mungu anatutarajia sisi kuwaruhusu wengine kutusaidia katika udhaifu wetu kwa kutumia uwezo aliyowapa.

Neno la Mungu iinasema Mungu amempa kila mmoja uwezo wa kipekee; zitumie kuwasaidia wengine, kuwapa wengine baraka nyingi za Mungu.

Vifaa vingi kama vile vikundi vya theluthi 3/3, vikundi vya uwajibikaji na Kushauriana Ki rika hutusaidia kuhimizana mmoja kwa mwenzake kiupendo na  kazi nzuri sio tu kutusaidia kutii yale Mungu anatueleza kufanya bali inatusaidia kupata njia ya kushiriki na wengine yale tuliyojifunza na wengine.

Mungu pia hutumia udhalimu na mateso – dhabihu na hasara tunayokabiliana nayo kwa ajili ya Yesu – kutufanya tukue kiroho.

Wakati watu wanatuhukumu na kutuumiza kwa sababu tunampenda na kumtii Yesu, ama wakati mambo mabaya yanatutokea pamoja na kwamba tunampenda na kumtii Yesu, Mungu hutumia huo udhalimu na mateso kuboresha tabia zetu kutufanya tuwe kama Yesu.

Yeye hustawisha tabia zetu, hutuimarisha na kutakasa imani yetu, hutuandaa kwa huduma na hutuwezesha kuhudumia wegine ambao wanateseka – wakati wote akijitambulisha waziwazi kwa kila mtu anayetutazama na kuelewa maumivu yetu.

Mungu anatueleza kwamba, kama wafuasi wa Yesu lazima tutarajie mateso.

Yesu alisema – Mungu atawabariki wakati watu wanakutukana, wanakutendea mabaya, na kusema kila aina uongo juu yenu kwa ajili yangu mimi. Kueni na furaha na msisimko! Mtakuwa na thawabu kubwa mbinguni. Watu waliwafanyia mambo hayo manabii ambao waliishi zamani.

Vifaa kama theluthi 3/3 vya vikundi vya uwajibikaji huwapa wafuasi wa Yesu fursa ya kushiriki udhalimu na mateso wanayopata.

Vikundi hivi vinawapa nafasi ya kufundisha wanafunzi kwamba neno la Mungu linasema tutarajie nyakati ngumu na kuwawezeshea njia ambazo

wanaweza kukabiliana nazo kwa kuamini upendo wake Mungu hata wakati mambo yanaenda mrama.

Maandiko. Maombi. Mwili Uzima. Udhalimu na Mateso.

Hivi ndivyo Mungu anatukuza tue bora zaidi kama mwanawe mkamilifu Yesu.

Vifaa vinavyotusaidia sio tu kwa watumiaji wa mambo haya mazuri ambayo Mungu ametupa bali kuwa wazalishaji na washirika pia

## JADILI

**(dakika 10)**

- Katika maeneo manne yaliyo hapo juu (maombi, Neno la Mungu, nk), ni ipi tayari unafanya?
- Ni zipi unahisi huna hakika nazo?
- Je! Unajisikia tayari kiasi wakati wa kufundisha wengine?

## SOMA

**Mfuatano wa Maombi**

Yesu mara nyingi aliwafundisha wafuasi wake kuhusu kusudi, zoezi na ahadi ya maombi.

Yesu alisema - “Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtapata; bisheni mlango, nanyi mtafunguliwa. Maana, yeyote aombaye hupewa, atafutaye hupata, na abishaye mlango hufunguliwa.”

Yesu alifundisha wafuasi wake kwamba maombi sio ya kusifiwa hadharani, orodha ya matamanio ya ubinafsi ama kupayuka tunayorudia tena na tena.

Yesu alitufundisha kwamba maombi yana nguvu kwa sababu ni majadiliano ya moja kwa moja na Baba yetu aliye mbinguni ambaye anatupenda.

Kama mazungumzo yoyote mazuri, maombi mazuri yanamaanisha pande zote mbili zinasikiliza – na kuongea.

Lakini kuongea na Mungu aliyeumba ulimwengu inawezakuwa ya kutisha. Na hasa kusikia jibu – kwa watu wengine hiyo inawezakuwa ya kutisha mno.

Habari njema ni kuwa mzuri kwa maombi – kuwa na maongezi bora na ya kindani na Mungu ambaye anatupenda – sio tu kwamba haiwezekani – ndio hivyo Mungu anataka hasa.

Wakati maombi yakionekana ni kama kujifunza lugha mpya – je, wawezaje kuwa bora?

Jibu ni rahisi – unajizoesha.

Mzunguko wa Maombi ni rahisi kwa kujizoesha kuomba ambayo unaweza kutumia wewe mwenyewe  na kushiriki na mfuasi yeyote.

Kwa hatua 12 rahisi – kwa dakika 5 – Mfuatano wa Maombi unakuongoza katika njia kumi na mbili ambayo Biblia inatufundisha kuomba.

Na mwisho, utakuwa umeomba kwa lisaa moja. Biblia inatueleza – "Omba bila kukoma."

Sio wengi wetu wanaweza kusema tunafanya hivyo. Lakini baada ya lisaa la maombi – utakuwa hatua moja karibu.

Mzunguko wa Maombi – Chombo kimoja rahisi katika mafundisho ya Zume.

## SHUGHULI


**(dakika 60)**

**Mfuatano wa Maombi**

- Omba Mzunguko wa Maombi kwa saa moja kibinafsi
- Tenga wakati wa kundi kurudi na kuunganika tena. Hakikisha kuongeza dakika chache zaidi kwa kila mtu kwa wote kupata nafasi ya utulivu kuomba na kurudi kwa kundi hilo.

**Maudhui:**

Kwa hatua 12 tu rahisi - dakika 5 kila moja - Mzunguko huu wa Maombi unakuongoza kupitia njia 12 ambazo Biblia inatufundisha kuomba. Mwishowe, utakuwa umeomba kwa saa moja.




**SIFA**

Anza saa yako ya maombi kwa kumsifu Bwana. Msifu kwa mambo ambayo yako akilini mwako sasa hivi. Msifu kwa jambo moja maalum ambalo amefanya katika maisha yako katika wiki iliyopita. Msifu kwa wema wake kwa familia yako.

**SUBIRI**

Tumia muda kumngoja Bwana. Nyamaza na umruhusu akuvute tafakari.

**UKIRI**

Mwombe Roho Mtakatifu akuonyeshe chochote katika maisha yako ambacho kinaweza kuwa hakimpendezi. Mwambie akuonyeshe mitazamo ambayo si sahihi, pamoja na matendo mahususi ambayo bado hujafanya maombi ya kuungama. Sasa ungameni hilo kwa Bwana ili mpate kutakaswa.

**SOMA NENO**

Tumia muda kusoma katika Zaburi, katika manabii, au vifungu vya maombi vilivyo katika Agano Jipya.

**ULIZA**

Fanya maombi kwa niaba yako mwenyewe.

**MAOMBI**

Fanya maombi kwa niaba ya wengine.

**OMBA NENO**

Omba vifungu maalum. Sala za Kimaandiko na vilevile Zaburi kadhaa hufaa kwa kusudi hilo.

**ASANTE**

Mshukuru Bwana kwa mambo katika maisha yako, kwa niaba ya familia yako, na kwa niaba ya kanisa lako.

**IMBA**

Imba nyimbo za sifa au kuabudu au wimbo mwingine au wimbo wa kiroho.

**TAFAKARI**

Mwombe Bwana aseme nawe. Kuwa na kalamu na karatasi tayari kurekodi hisia Anazokupa.

**SIKILIZA**

Tumia muda kuunganisha mambo ambayo umesoma, mambo ambayo umeomba na mambo ambayo umeimba na uone jinsi Bwana anavyovileta pamoja ili kuzungumza nawe.

**SIFA**

Msifu Bwana kwa muda ambao umekuwa naye na hisia ambazo amekupa. Msifuni kwa sifa zake tukufu.

Kutoka kwenye kitabu cha Dick Eastman cha The Hour that Changes the World © 2002 na Dick Eastman, Chosen Books, Grand Rapids, MI, kilichotumiwa kwa ruhusa.

## JADILI

**(dakika 10)**

- Je, unaonaje kutumia lisali moja kwa maombi?
- Unahisi aje?
- Ulijifunza au kusikia chochote?
- Je! Maisha yangekuwaje kama ungefanya maombi ya aina hii kuwa kawaida?

## SOMA

**(Dakika 5)**

**Orodha ya 100**

Yesu alisema - “Nendeni mkawafanye wanafunzi…” Na wafuasi wake wakafanya vivyo hivyo.

Walienda kwa jamaa zao. Walienda kwa marafiki zao. Walienda kwa wale watu waliowajua mjini. Walienda kwa wale watu waliofanya kazi pamoja nao. Walienda.

Yesu alisema “Nendeni” na walitii. Na familia yake Mungu ikakua

Mungu tayari ametupa uhusiano tunaohitaji “Nendeni mkawafanye wanafunzi.”

Hawa ni jamaa zetu, marafiki, majirani, wafanyi kazi wenzetu na tunaosoma nao – watu ambao tumewajua maishani mwetu wote, watu ambao tumekutana tu nao

Kuwa waaminifu kwa watu ambao Mungu tayari amewaweka katika maisha yetu ni hatua kuu ya kwanza ya kuzidisha wanafunzi. Na inaweza kuanza na hatua rahisi sana ya kuandiko tu orodha.

Orodha ya 100 ni mafundisho katika Zume ambayo inazidisha wanafunzi

## SHUGHULI

**(dakika 30)**

**Tengeneza orodha yako mwenyewe ya mia moja**

- Acha kila mtu katika kikundi chako achukue dakika 30 zijazo kujaza orodha yao ya mahusiano. Orodhesha nyingi uwezavyo.
- Kisha weka alama ufahamu wako bora zaidi wa uhusiano wao na Mungu: mfuasi, asiyeamini, au asiyejulikana.

1 ______________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

2 ______________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

3 ______________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

4 ______________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

5 ______________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

6 ______________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

7 ______________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

8 ______________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

9 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

10 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

11 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

12 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

13 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

14 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

15 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

16 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

17 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

18 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

19 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

20 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

21 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

22 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

23 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

24 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

25 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

26 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

27 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

28 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

29 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

30 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

31 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

32 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

33 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

34 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

35 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

36 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

37 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

38 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

39 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

40 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

41 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

42 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

43 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

44 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

45 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

46 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

47 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

48 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

49 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

50 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

51 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

52 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

53 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

54 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

55 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

56 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

57 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

58 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

59 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

60 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

61 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

62 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

63 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

64 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

65 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

66 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

67 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

68 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

69 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

70 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

71 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

72 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

73 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

74 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

75 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

76 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

77 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

78 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

79 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

80 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

81 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

82 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

83 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

84 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

85 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

86 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

87 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

88 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

89 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

90 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

91 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

92 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

93 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

94 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

95 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

96 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

97 ________________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

98 ______________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

99 ______________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

100 ______________________ ☐ Mwanafunzi ☐ Asiyeamini ☐ Haijulikani

## ANGALIA

**(dakika 1)**

**Dhana zilizosikika katika kikao hiki:**

- Mtayarishaji Sio Mtumiaji

**Zana zilizosikika katika kikao hiki:**

- Mfuatano wa Maombi
- Orodha ya 100

### HATUA IFUATAYO

## TII

Tumia wakati juma hili ukiombea watu watano kutoka kwenye Orodha yako ya 100 uliyoweka alama kama "Wasioamini" au "Hajulikani." Muombe Mungu aandae mioyo yao kuwa wazi kwa hadithi Yake.

## SHIRIKI

Muulize Mungu kuhusu yule anataka ushiriki naye Orodha ya 100. Shiriki jina la mtu huyu na kundi kabla ya kwenda na kuwafikia kabla ya kipindi kijacho.

KIKAO CHA 3

## INGIA

**(dakika 1)**

Waruhusu washiriki wote na mwezeshaji waingie.

Au zume.training/checkin na utumie msimbo: **6543**

## OMBA

**(Dakika 5)**

Omba na kumshukuru Mungu kwa njia ulizopitia Yeye katika kipindi kilichopita na mwalike Roho Wake Mtakatifu kuongoza wakati wako pamoja.

## ANGALIA NYUMA

**(Dakika 5)**

Kabla ya kuanza, chukua muda kutazama nyuma.

Mwishoni mwa kipindi kilichopita, kila mtu katika kikundi chako alipewa changamoto ya kufanya mazoezi uliyojifunza.

Chukua muda mfupi kuona jinsi kundi lako lilivyofanya juma hili.

## MAPITIO

**(dakika 1)**

**Katika kikao hiki, tutasikia na kujadili dhana hii:**

- Uchumi wa Kiroho

**Na tutaongeza zana hizi kwenye seti yetu ya zana:**

- Injili
- Ubatizo

## SOMA

**(Dakika 5)**

**Uchumi wa Kiroho**

Katika kikao hiki, tutaongea kuhusu UCHUMI wa KIROHO wa Mungu. Katika ulimwengu huu, watu wanajihisi wamezawadiwa wanapochukua, wanapopokea na wanapofaidika kuliko wenzao walio karibu nao.

Katika maandiko yake, Mungu anawaambia watu wake – Mawazo yangu sio mawazo yenu, wala njia zangu sio njia zenu.

Mungu anatuonyesha kwamba katika uchumi wake wa Ufalme, tunazawadiwa sio kwa kile tunachopata – bali kwa kile kutoa.

Mungu anasema – nitawaokoa, nanyi mtakuwa baraka. Yesu anasema – Heri kutoa kuliko kupokea. Kutoa yale Mungu ametupa na kuwabariki wengine wakati Mungu anatubariki ni msingi wa KUPUMUA KIROHO tuliojifunza hapo awali.

Tunapumua NDANI na KUSIKIA kutoka kwa Mungu. Tunapumua NJE na KUTII yale tuliyoyasikia na KUSHIRIKI na wengine.

Tukiwa waaminifu KUTII na KUSHIRIKIANA yale BWANA ameshiriki nasi, basi hapo anaahidi kushiriki hata zaidi.

Yesu alisema – anayeweza kuaminiwa kwa vicache anaweza kuaminiwa kwa vingi. Hii ndiyo njia ya kufahamu kwa udani, ushirika wa karibu na kuishi maisha tele aliyotuumba Mungu tuyaishi. Hii ndio njia tunayoweza

kutembea kutembea katika matendo  mema ambayo Mungu ametupangia kufanya.

Ikiwa tunahitaji kuzawadiwa na zawadi kuu ya Mungu, Basi lazima tujizoeshe kwa mambo mawili aliyoahidi kubariki.

Ni lazima -

- KUTII na KUSHIRIKIANA
- FANYA na KUFUNDISHA
- JIZOESHE na UPOKEZANE

-kila kitu Mungu anakueleza tukafanye.

Ikiwa tunataka wengine nao wapokee zawadi kuu ya Mungu, basi ni lazima tuwaonyeshe jinsi ya kufanya mambo hayo, pia. Hi ni sehemu muhimu ya kuwa mwanafunzi na sehemu muhimu ya kuwafanya wanfunzi.

- Sisi ni WAFUASI  na VIONGOZI
- WANAFUNZI na WALIMU
- TUMEBARIKIWA  na sisi ni BARAKA

Mungu hataki tungojee hadi tumeelewa kila kitu kabla tuanze kutii na kushirikiana. Siku hiyo haitafika.

Mungu hatutarajii tukomae kabisa kabla tuanze kujizidisha. Anataka tujizidishe mara moja. Mungu anataka tutii yale tumejua tayari na kushirikiana yale tuliyoyasikia tayari.

Na kisha anataka tuwafundishe wengine kufanya hivyo. Baada ya yote – hiyo ni kutii na kushirikiana yale alituambia tukafanye. Hii ndio njia ya ukomavu na ukuaji.

## JADILI

**(dakika 10)**

Je, ni tofauti gani unazoona kati ya Uchumi wa Kiroho wa Mungu na njia yetu ya kidunia ya kufanya mambo kutendeka?

**Yesu alisema, “Mtapokea nguvu akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu. Nanyi mtakuwa mashahidi wangu, mkihubiri habari zangu kila mahali, katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata miisho ya dunia."**

Hakuna "njia bora zaidi" ya kusimulia hadithi ya Mungu (pia inaitwa Injili), kwa sababu njia bora itategemea nani unashiriki naye. Kila mwanafunzi anapaswa kujifunza kuelezea Hadithi ya Mungu kwa njia ambayo ni kweli kwa maandiko na inaeleweka kwa wasikilizaji wanaowashiriki.

## JADILI

**(dakika 10)**

- Kitu gani hukujia mawazoni unaposikia amri ya Mungu ya kuwa "shahidi" wake na kusimulia hadithi yake?
- Kwa nini unafikiri Yesu alichagua watu wa kawaida badala ya njia nyingine ya kushiriki habari zake njema?
- Je! Itachukua nini kwa wewe kujihisi vizuri kushiriki hadithi ya Mungu?

## SOMA

**(Dakika 5)**

**Injili**

Katika kikao hiki, tutajifunza jinsi ya kushirikiana HADITHI ya MUNGU – INJILI - kutoka Uumbaji hadi Hukumu, tangu mwanzo wa wanadamu hadi mwisho wa nyakati. Kuna njia nyingi za kushiriki hadithi ya Mungu.

Njia bora zaidi itategemea mtu unayeshiriki naye na maoni yake kuhusu ulimwengu na uzoefu wake wa kimaisha.

Mungu hutumia mioyo yenye nia ya kushiriki kutenda kwa mioyo yenye nia ya kusikia.

Ni kazi yake. Anatualika tu tukajiunge naye.

Njia moja ya kushiriki hadithi ya Mungu ni kwa kuelezea kilichotokea tangu Uumbaji hadi kwenye Hukumu mwa nyakati hizi.

Tunaposema hadithi ya Mungu kwa njia hii, tunaweza kuurefusha au kuufupisha, kwa kina au fupi fupi lakini iwe imeunganika na utamaduni wa mwenye anakusikiza.

Ili kusaidia kuelezea Hadithi Yake katika tamaduni tofauti na maoni ya ulimwengu, unaweza pia kuonyesha kwa mkono ambao hufanya iwe rahisi kujifunza na kufundisha.

Hapa kuna Hadithi ya Mungu ya Habari Njema -

Hapo mwanzo, Mungu aliumba ulimwengu na  vitu vyote.

Aliumba MWANAUME wa KWANZA na MWANAMKE wa KWANZA.

Akawaweka kwenye bustani nzuri. Aliwafanya kuwa SEHEHMU ya FAMILIA YAKE na UHUSIANO WA KARIBU pamoja nao.

Aliwaumba WAWEZE KUISHI pamoja. Hapakuwa kitu kama kifo.

Hata katika mahali hapa, mwanadamu alimuasi Mungu na kuleta DHAMBI na MATESO duniani.

Mungu akamfukuza mwanadamu kutoka kwenye bustani. Uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu ukakatizwa.

Sasa ikawa mwanadamu lazima afe.

Zaidi ya mamia ya miaka, Mungu alizidi kuwatuma WAJUMBE duniani. Waliwakumbusha wanadamu dhambi zao na pia kuwaeleza kuhusu UAMINIFU wa Mungu na AHADI zake za kumtuma MWOKOZI duniani.

Mwokozi angerejesha uhusiano wa karibu kati ya Mungu na wanadamu, mwokozi angemuokoa mwanadamu kutoka kwa kifo. Mwokozi atapeana uzima wa milele na kuokoa mwanadamu milele.

Mungu anatupenda sana hata wakati ulipotimia, alimtuma Mwanawe duniani ili awe yule Mwokozi.

Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Alizaliwa duniani kupitia bikira. Aliishi maisha makamilifu. Hakutenda dhambi.

Yesu aliwafundisha watu kuhusu Mungu. Alitenda miujiza mingi kudhihirisha uwezo wake. Alikemea pepo wengi. Aliponya watu wengi. Aliwafanya vipofu kuona. Aliwafanya viziwi kusikia. Aliwafanya viwete kutembea.

Yesu hata aliwafufua wafu. Viongozi wengi wa dini WALIHOFIA sana na kumchukia Yesu. Walitaka kumuua.

Kwa vile hakutenda dhambi, hakustahili kufa. Lakini ALIAMUA kufa kama DHABIHU kwetu sote. Kifo chake kilifunika dhambi za mwanadamu.

Baada ya haya, Yesu alizikwa kaburini.

Mungu aliona DHABIHU yake Yesu na kukubali. Mungu alionyesha kukubali kwake kwa kumfufua Yesu kutoka wafu siku ya tatu.

Mungu alisemba kwamba ikiwa TUTAAMINI na KUMPOKEA Yesu kama dhabihu ya dhambi zetu – TUKIACHANA na dhambi na KUMFUATA Yesu, Mungu HUTUTAKASA kwa dhambi zote na KUTUKARIBISHA tena katika jamaa yake.

Mungu humtuma ROHO MTAKATIFU aishi ndani mwetu na kutusaidia kumfuata Yesu.

TUNABATIZWA kwa maji kuonyesha na kuidhinisha uhusiano huu uliorejeshwa.

Kama ishara ya kifo tunazikwa ndani ya maji. Kama ishara ya maisha mpya tunainuliwa kutoka majini kumfuata Yesu. Wakati Yesu alipofufuka kutoka wafu, alikaa duniani siku arobaini.

Yesu aliwafundisha wafuasi wake kwenda kila mahali kufundisha kila mtu kuhusu habari njema ya wokovu wake.

Yesu alisema – NENDENI na MKAWAFANYE WANAFUZI mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwa BATIZA, kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na KUWAFUNDISHA kuyashika yote niliyowaamuru ninyi, tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata mwisho wa dahari.

Yesu AKAINULIWA juu mbele ya macho yao hata mbinguni. Siku moja, Yesu ATAKUJA TENA kwa njia hiyo hiyo.

Atawaadhibu milele wote ambao hawakumpenda na kumtii.

ATAWAPOKEA na KUWAZAWADI MILELE wote waliompenda na kumtii.

TUTAISHI MILELE pamoja naye katika Mbingu Mpya na Dunia Mpya.

NILIAMINI na NIKAPOKEA dhabihu iliyoandaliwa na Yesu kwa ajili ya dhambi zangu. Alinifanya kuwa msafi na kunirejesha kama sehemu ya jamaa ya Mungu. Ananipenda, nami nampenda milele katika ufalme wake.

Mungu anakupenda na anataka ukaipokee zawadi hii, pia. Je, ungependa kufanya hivyo sasa hivi?

## JADILI

**(dakika 10)**

- Unajifunza nini kumhusu mwanadamu kutoka kwa hadithi hii?
- Unajifunza nini kumhusu Mungu?
- Je, unafikiri itakuwa rahisi au vigumu kwa kushiriki Hadithi ya Mungu kwa njia hii?

## SHUGHULI

**(dakika 45)**

**Shiriki Injili**

- Gawanya katika vikundi vya watu wawili au watatu.
- Mpeane zamu ya kuelezana Injili.

**Maudhui:**

**Hadithi ya Mungu: Mtindo wa Uumbaji hadi Hukumu**

Hapo mwanzo, Mungu aliumba ulimwengu wote na vyote vilivyomo.

Alimuumba MWANAUME WA KWANZA na MWANAMKE WA KWANZA. Akawaweka katika bustani nzuri. Aliwafanya kuwa SEHEMU YA FAMILIA YAKE na kuwa na UHUSIANO WA KARIBU nao.

Aliwaumba WAISHI MILELE. Hakukuwa na kitu kama kifo. Hata mahali hapa pazuri, mwanadamu alimuasi Mungu na kuleta DHAMBI na MATESO duniani. Mungu AKAMFUKUZA mtu kutoka bustanini. Uhusiano kati ya mwanadamu na Mungu ULIVUNJIKA. Sasa mwanadamu angekabiliana na MAUTI. Zaidi ya mamia ya miaka, Mungu aliendelea kutuma WAJUMBE duniani. Walimkumbusha mwanadamu dhambi yake lakini pia walimwambia juu ya UAMINIFU na AHADI ya Mungu ya kutuma MWOKOZI duniani.

Mwokozi Angeweza KURUDISHA uhusiano wa karibu kati ya Mungu na Mwanadamu. Mwokozi angemkomboa mwanadamu kutoka kwa kifo. Mwokozi angetoa UZIMA WA MILELE na kuwa na mwanadamu milele. Mungu anatupenda sana hata wakati ulipowadia, alimtuma Mwanawe ulimwenguni kuwa Mwokozi huyo.

Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Alizaliwa ulimwenguni kupitia bikira. Aliishi maisha makamilifu. Hakutenda dhambi kamwe. Yesu aliwafundisha watu kuhusu Mungu. Alifanya miujiza mingi akionyesha uwezo wake mkuu. Alitoa pepo wengi. Aliponya watu wengi. Aliwafanya vipofu waone. Aliwafanya viziwi wasikie. Aliwafanya viwete watembee. Yesu hata alifufua wafu. Viongozi wengi wa kidini WALITISHIWA na KUMWONEA WIVU Yesu.

Walitaka auawe. Kwa kuwa hakuwahi kutenda dhambi, Yesu hakupaswa kufa.

Lakini ALICHAGUA kufa kama SADAKA kwa ajili yetu sote. Kifo chake chenye uchungu kilifunika dhambi za wanadamu. Baada ya hayo, Yesu alizikwa kaburini. Mungu aliiona SADAKA ambayo Yesu aliitoa na kuikubali. Mungu alionyesha kukubalika kwake kwa kumfufua Yesu kutoka kwa wafu siku ya tatu.

Mungu alisema kwamba ikiwa TUNAAMINI na KUPOKEA dhabihu ya Yesu kwa ajili ya dhambi zetu -- Tukigeukia mbali dhambi zetu na KUMFUATA Yesu, Mungu ANATUTAKASA kutoka kwa dhambi zote na ANATUKARIBISHA tena katika familia yake.

Mungu humtuma ROHO MTAKATIFU kukaa ndani yetu na kutufanya tuweze kumfuata Yesu. TUMEBATIZWA katika maji ili kuonyesha na kuweka muhuri uhusiano huu uliorejeshwa.

Kama ishara ya kifo tunazikwa chini ya maji. Kama ishara ya maisha mapya tunainuliwa kutoka majini ili kumfuata Yesu.

Yesu alipofufuka kutoka kwa wafu, alitumia siku 40 duniani.

Yesu aliwafundisha wafuasi wake kwenda kila mahali na kutangaza habari njema ya wokovu wake kwa kila mtu ulimwenguni kote. Yesu alisema - Enendeni, MKAWAFANYE mataifa yote KUWA WANAFUNZI, MKIWABATIZA kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu; na KUWAFUNDISHA kuyashika yote niliyowaamuru. nitakuwa pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.

Ndipo Yesu ALIPULIWA Mbinguni mbele ya macho yao. Siku moja, Yesu ATARUDI TENA kwa njia ile ile aliyotoka. Atawaadhibu MILELE wale ambao hawakumpenda na kumtii. Atawapokea na kuwathawabisha MILELE wale waliompenda na kumtii. TUTAISHI MILELE pamoja Naye katika Mbingu Mpya na katika Dunia Mpya.

NILIAMINI na KUPOKEA dhabihu aliyoitoa Yesu kwa ajili ya dhambi zangu. Amenifanya kuwa safi na kunirudisha kama sehemu ya familia ya Mungu. Ananipenda, na ninampenda na nitaishi naye milele katika ufalme Wake. Mungu anakupenda na anataka upokee zawadi hii pia. Je, ungependa kufanya hivyo sasa hivi?

Fanya mazoezi ya uwasilishaji huu wa injili peke yako hadi uhisi vizuri kusimulia hadithi.

---

## SOMA

**(Dakika 5)**

**Ubatizo**

Yesu alisema--”nenda mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi,mkiwabatiza kwa jina la Baba, la Mwana  na la Roho mtakatifu...”

Ubatizo -au Baptizo kwa lugha asilia -inamaanisha ni mfereji au iliyojaa -vile unavyo zamisha nguo ndani ya rangi na unaapoitoa ndani hubadilika.

Ubatizo ni taswira ya maisha mapya.yamezamishwa kwa mfano wa Kristo,kwa kubadilishwa kwa njia ya kutii Mungu. Ni taswira ya mauti yetu kwa dhambi,kama vile Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu,kuzika mwili wetu wa kitambo, kama vile Kristo alivyozikwa;ni kuzaliwa upya katika maisha mapya ya Kristo,vile Kristo alivyofufuka na anaishi sasa.

Ikiwa hujawahi batiza mtu yeyote,huenda ikaonekana kama udhalilishaji,ila hivyo sivyo,hapa kuna hatua chache za kufuata.

Tafuta maji yaliyotulia, yaliyo na kina kirefu yanayoruhusu mwanafunzi kuzamishwa.Iwe ni bwawa,mto,ziwa au bahari.Iwe ni bafu ama njia nyingine za kukusanya maji.

Wacha mwanafunzi mmoja ashikilie mkono wako kwa mkono wake na kusaidiwa na mwingine.

Uliza maswali mawili jinsi hii ili kuhakikisha wameelewa maamuzi yao.

- “Umempokea Yesu kama mwokozi wa maisha yako?”
- “Utamtii na kumhudumia Mungu kama mfalme katika maisha yako yote yaliyosalia?”

Ikiwa watajibu “Ndiyo”kwa zote sema hivi:

- “Sababu umeweka imani yako kwa Kristo Bwana wetu,sasa nakubatiza kwa jina la Baba la Mwana na la Roho mtakatifu.”

Wasaidie kuinama ndani ya maji,zamisha mwili wote na uwainue wote tena.

Umebatiza mfuasi mpya wa Yesu-raia mpya wa mbingu-kiumbe kipya cha Mungu aishie.Ni wakati sasa wa kusherehekea!

Ubatizo-ni mkate wa kwanza Yesu aliwapa wafuasi wake na kuwa ni msingi wa kifaa cha Zume.

## JADILI

**(dakika 10)**

- Je, umewahi kubatiza mtu?
- Je! Unaweza kufikiria kufanya hivyo?
- Ikiwa Agizo Kuu ni kwa kila mfuasi wa Yesu, je, hiyo inamaanisha kila mfuasi anaruhusiwa kubatiza wengine? Kwa nini au kwa nini?

**Umuhimu wa anayekukumbusha-Umekua ukibatizwa?**

Ikiwa sivyo, basi tunakuhimiza upange hili kabla hata ya kipindi kimoja zaidi cha mafunzo haya. Alika kikundi chako kuwa sehemu ya siku hii muhimu unaposherehekea kusema "ndiyo" kwa Yesu.

## ANGALIA

**(dakika 1)**

**Dhana zilizosikika katika kikao hiki:**

- Uchumi wa Kiroho

**Zana zilizosikika katika kikao hiki:**

- Injili
- Ubatizo

### HATUA IFUATAYO

## TII

Muulize Mungu kuhusu mtu yule anataka ufundishe kutumia Uumbaji kwenye hadithi ya Hukumu (au njia nyingine ya kushiriki hadithi ya Mungu). Shirikisha jina la mtu huyu na kundi kabla ya kwenda.

## SHIRIKISHA

Tumia muda juma hili ukijizoeza Hadithi ya Mungu, kisha uishiriki na angalau mtu mmoja kutoka kwenye Orodha yako ya 100 uliyoweka alama kama "Wasioamini" au "Hajulikani."

**UZURI WA ANAYEKUKUMBUSHA-Kundi lako litasherehekea Meza ya Bwana awamu inayokuja.Kuwa na hakika kusambaza(mikate na divai/mvinyo).**

# KIKAO CHA 4

## INGIA
**(dakika 1)**

Waruhusu washiriki wote na mwezeshaji waingie.

Au zume.training/checkin na utumie msimbo: **8764**

## OMBA
**(Dakika 5)**

Omba na kumshukuru Mungu kwamba anatualika kushiriki Habari Njema Yake na wengine.

Mwombe akupe kila mshiriki wa kikundi chako mawazo ya Kristo - na kujaza kila mmoja na Roho Wake.

## ANGALIA NYUMA
**(Dakika 5)**

Kabla ya kuanza, chukua muda kutazama nyuma.

Mwishoni mwa kipindi kilichopita, kila mtu katika kikundi chako alipewa changamoto ya kufanya mazoezi uliyojifunza.

Chukua muda mfupi kuona jinsi kundi lako lilivyofanya juma hili.

## MAPITIO

**(dakika 1)**

**Katika somo hili, tutasikia na kujadili dhana hizi:**

- Maono Kutupa Baraka Kubwa Zaidi
- Uwanafunzi wa Watoto wa Bata
- Macho ya Kuona penye Ufalme Hauko

**Na tutaongeza zana hizi kwenye seti yetu ya zana:**

- Ushuhuda wa Dakika Tatu
- Meza ya Bwana

## SOMA

**(Dakika 5)**

**Ushuhuda wa Dakika Tatu**

Yesu aliwaambia wafuasi wake- “Ninyi mashahidi wa vitu hivi”

Kama mashahidi wa Yesu Kristo sisi ni “mashahidi” pia-”kushuhudia”matokeo ambayo Yesu ametufanyia maishani mwetu.

Hadithi yako kuhusu uhusiano wako na Mungu unaitwa ushuhuda.

Kila mmoja ana hadithi.Hii ni nafasi ya kufanyia mazoezi hadithi yako.

Chagua mfuasi mmoja au wawili kufanya nao mazoezi na halafu chagua majina matano kutoka kwa orodha ya watu mia moja.

Hakikisha unachagua watu kimakundi “siwakristo”au ambao hawajulikani kiroho.”

Fanyia mazoezi ushuhuda wako-hadithi yako juu ya Yesu kuwa na wale mnaofanya nao mazoezi huku ukijifanya mmoja wa wale watano kutoka orodha yako.

Fanya mazoezi uione hadithi yako na kuifanya spesheli kwa kila mmoja wa hao watano.

Unaweza kuwasimulia hadithi yako kwa mtindo wa dakika tatu.

Kuna njia nyingi za kuboresha hadithi yako ,ila kuna baadhi ya njia tumeona zimetumika vizuri kwa wengine;

Unaweza simulia taarifa fupi kwa nini watu wanafuata Yesu.Hii inafanyika vyema kwa muumini mpya.

Unaweza elezea hadithi yako ya Maisha yako kabla na baada ya kumfahamu Yesu na vile maisha yako yalivyo wakati huu. Rahisi na yenye nguvu ajabu.

Unaweza simulia hadithi yako “kuwa na” au “bila” Yesu katika maisha yako na kipi kitakuwa bila Yesu. Mtindo huu wako unafanikiwa ikiwa unaanzia imani ya ukiwa na umri mdogo.

Wakati unapomaliza kuwaelezea, wacha mnaofanya mazoezi nao pamoja kusimulia pia hadithi yao. Endelea hadi wamalize wote watano.

Unataka kupata matokeo makubwa zaidi?

Unaposimula hadithi yako,ni muhimu kuwaza juu yake kama njia moja ya mchakato:

- Hadithi yako-Uliza mtu mnaoongea pamoja kusimuliua kuhusu safari yao ya kiroho.
- Hadithi yako-Simulia ushuhuda wako karibu na mazingira yako.
- Hadithi ya Mungu-Hatimaye kuzungumzia hadithi ya Mungu kwa njia ya kuunganisha mtazamo wao wa ulimwengu,thamani na nafasi.

Na ikiwa unashangazwa kuhusu vile utaanza-fanya iwe rahisi.

Elezea kwa taarifa vile uliamua kumfuata Yesu.

Mungu anaweza kutumia hadithi yako kubadilisha maisha, lakini kumbuka-ni wewe mwenyewe unastahili kuwaambia hiyo hadithi.

Ushuhuda wako wa dakika tatu ni kifaa katika vifaa vya Zume.

## SHUGHULI

**(dakika 30)**

**Jizoeze kushiriki ushuhuda wako**

- Fanya kazi katika kuandika hadithi yako na ihifadhi kwa dakika tatu tu. (dakika 10)
- Gawa katika vikundi vya watu wawili hadi watatu na ufanye mazoezi ya kushiriki. (Dakika 20)

**Maudhui:**
**Aina Tatu za Msingi za Ushuhuda**

Kuna njia nyingi za kuunda hadithi yako, lakini hizi ni baadhi ya njia ambazo tumeona zikifanya kazi vizuri:

- Taarifa Rahisi - Unaweza kushiriki taarifa rahisi kuhusu kwa nini ulichagua kumfuata Yesu. Hii inafanya kazi vizuri kwa muumini mpya kabisa.
- Kabla na Baada - Unaweza kushiriki hadithi yako "kabla" na "baada ya" - maisha yako yalikuwaje kabla ya kumjua Yesu na maisha yako yalivyo sasa. Rahisi na yenye nguvu.
- Pamoja na Bila - Unaweza kushiriki hadithi yako ya "na" na "bila" - maisha yako yalivyo "pamoja na Yesu" na jinsi ingekuwa "bila Yeye". Toleo hili la hadithi yako hufanya kazi vizuri ikiwa ulikuja kuamini katika umri mdogo.

**Sehemu Tatu za Kushiriki Ushuhuda Wako**

Unaposhiriki hadithi yako, ni muhimu kuifikiria kama sehemu ya mchakato wa sehemu tatu:

- Hadithi Yao - Uliza mtu unayezungumza naye kushiriki kuhusu safari yao ya kiroho.
- Hadithi Yako - Kisha shiriki Ushuhuda wako kulingana na uzoefu wao.
- Hadithi ya Mungu - Hatimaye shiriki hadithi ya Mungu kwa njia inayounganishwa na mtazamo wao wa ulimwengu, maadili na vipaumbele.

Si lazima Ushuhuda wako uwe mrefu au ushiriki maelezo mengi ili uweze kuleta matokeo. Kwa kweli, kuhifadhi hadithi yako kwa takriban dakika 3 kutaacha wakati wa maswali na mazungumzo ya kina. Ikiwa una wasiwasi kuhusu jinsi ya kuanza - iwe rahisi. Mungu anaweza kutumia hadithi yako kubadilisha maisha, lakini kumbuka - wewe ndiye unayeweza kuisimulia.

## SOMA

**(Dakika 5)**

**Kubwa - Kubwa - Baraka Kubwa**

Katika awamu hii, tutazungumzia kuhusu ukuu wa Mungu, ukuu zaidi na Baraka kuu na vile utakavyowapa wengine Baraka hizo. Wakati mtu anapochagua kumfuata Yesu, unamsaidiaje kwa kupata mwongozo kwa njia iliyo sawa?

Unawasaidiaje kuwa wazalishaji katika ufalme wa Mungu na siwatumiaji?

Unawasiadiaje kupokea baraka yote ambayo Mungu anapendelea kuwapa?

Ninaanza kwa kuwambia hivi…

- Ni Baraka kumfuata Yesu.
- Ni Baraka kuu kuwaongoza wengine kumfuata Yesu.
- Ni Baraka kuu kuanza familia mpya ya kiroho.
- Ni Baraka iliyo kuu zaidi kuandaa wengine kuanza familia mpya za kiroho.

Umechagua kumfuata Yesu na Mungu amekubariki.

Nahitaji upokee Baraka za Mungu, Baraka kuu, Baraka kuu mno, zaidi pia. Naweza kukuonyesha.

Ikiwa wanahitaji kufahamu zaidi, nitahitaji wao kutengeneza orodha ya watu 100 ambao tayari wanawafahamu.

Baadaye nitawauliza kuchagua watu watano kutoka kwa orodha hiyo watu watano ambao hawamjui  Yesu, watano wangependa kushiriki neno mara moja.

Ni Baraka kufuata Yesu. Ungemshirikisha nani tena katika Baraka hizi?

Nawafundisha jinsi ya kutoa ushuhuda – na hadithi ya vile Mungu anafanyakazi katika maisha yao – Nawapa maelekezo ya kueneza injili- hadith kuhusu kile Mungu amefanya duniani. Nawafundisha kuhusu Baraka za Mungu zilivyo kuu, kuu zaidi, na ajabu.

Nitahitaji kuwapa mazoezi ya kufanya kwa kila kundi la watu watano walio wachagua kushiriki nao. Kwanza kuhusu hadithi yao wenyewe. Halafu hadithi kuhusu Mungu. Hatimaye baraka za Mungu.

Kila wakati najifanya kuwa mmoja wa hao watano walio katika orodha yao.

Kila wakati wanaelezea hadithi yao. Wanaelezea hadithi kuhusu Mungu. Wananialika kuwa mfuasi wa Yesu pia. Wanafundisha kuhusu ukuu wa Mungu,  ukuu zaidi, na Baraka za Mungu pia.

Kila wakati nawahoji ili kupata mapendekezo ambayo nafikiria mtu anaweza kupendekeza. Baada ya mazoezi, nawaomba tukutane tena- ikiwezekana siku mbili baadaye- ili kutaathimini mwendo wao unavyoendelea.

Nahitaji kuwapa muda wa kutosha ili kukutana na watu watano walio waorodhesha, ila sitaki kuwapa muda mrefu wasije wakasahau na kufutilia mbali hatua hiyo.

Siku zote nawaomba anuani yao au namba ya simu ili kuendelea kuwasiliana nao.

Naomba pamoja nao ili Mungu awape maneno sahihi vile wanavyoendelea kushiriki nami.

Siku mbili baadaye, tunakutana na kuwa na mazungumzo nao kuhusu vile wanavyoendelea kushiriki.

Ikiwa hawajashirikisha wengine, najitolea kufanya mazoezi nao. Najitolea kutembea nao ikiwa wale watano inawezekana wawemo. Nafanya kulingana na uwezo wangu ili kuwafanya waanze kushiriki.

Ila sitazungumzia vitu vipya. Nitawapa muda unaofaa wa kuwa waaminifu kwa yale wamejifunza.

Ikiwa watakataa au kuwa visingizi, ninaomba Mungu ikiwa ni kweli “udongo warutuba” ambao utazalisha katika ufalme wake au ikiwa kuna mwingine sehemu nyingine ambapo naweza kuwekeza.

Ikiwa walishirikisha wengine –tunasherekea.

Hata kama hakuna katika orodha hiyo ambaye hakuamini, ninafurahia maana WAMESIKIA KUTII na KUSHIRIKISHA WENGINE. Hapo ni kuwa mwaminifu.

Na vile wamekua waaminifu kwa vichache, ninafurahia kuwapa zaidi.

Nawafundisha kuhusu UBATIZO na kuwapa silaha nyingine wanaweza kutumia kama njia ya mambo na kubuni kikundi kuwauliza kuchagua watu wengine kutoka orodha ya watu mia moja- watu ambao hawamjui au hawamfuati Yesu.

Baadaye nafanya mazoezi nao kama awali – na hadithi yao na ya Mungu na Baraka za Mungu. Halafu tunaomba.

Sasa ikiwa watajadiliana na mmoja wao aamini katika orodha hiyo basi kwa kweli TUTASHEREHEKEA!

Familia ya Mungu inaendelea kukuwa kubwa.

Mara kwa mara nawauliza ikiwa wamezungumzia Baraka kuu, kuu na kuu mno sababu hii ndio hufanya familia ya Mungu kukua.

Ikiwa hawakuzumgumzia kuhusu Baraka za Mungu, basi tunaanza tena —Baraka, jinsi gani mfuasi mpya wa Yesu anaweza kutengeneza orodha, wanawezaje kuzungumzia hadithi zao, zungumzia Mungu na Baraka za Mungu—vivyo hivyo mwanafunzi wa Yesu anaweza kujifunza na kuzungumzia pia.

Hatimaye baada ya kufanya mazoezi, nawatuma tena kwa waumini wapya ili waweze kuendelea kushiriki nao.

Na inakuaje kwa yule ambaye ameshiriki na mmoja katika orodha hiyo ameamini na walizungumzia kuhusu mibaraka?

Ikiwa yanafanyika ninajawa na FURAHA SANA.

Watu kama hawa neno la Mungu linawaita “udongo wa rutuba”—yeyote anayekua katika njia ya familia ya Mungu ni wakuu kuliko vile sijawahi waona.

Popote ninapopata mtu kama huyu, nafanya mpango wakukutana nao. Ninawekeza zaidi katika kukua kwao kwa kiroho.

Nawafundisha somo jipya kama UBATIZO na jinsi ya kuanza THELUTHI TATU ya makundi. Sasa wanaweza anza kukua familia ya kiroho-kwanza kwa wale waumini wapya wa Yesu.

Vile walivyo waaminifu, nimejawa na furaha kuzungumza zaidi kulingana na uwezo wangu na kuona kile ambacho Mungu atafanya baadaye. Siku zote hatua moja kwa wakati mmoja. Siku zote nawapa muda wakujifunza, kutii na kuwapa wengine kile wanachojua.

Pia ninaomba na mtu huyu-kulingana na uwezo wangu-Na kushukuru Mungu kuniruhusu kushiriki na kujifunza nao na daima kuomba Mungu kuwapa wote baraka zake kuu.

## JADILI

**(dakika 10)**

- Je, huu ndio kielelezo ulichofundishwa ulipoanza kumfuata Yesu kwa mara ya kwanza? Ikiwa sivyo, ni nini kilikuwa tofauti?
- Baada ya kuwa mwenye Imani, ilikuchukua muda gani kabla uanze kuwafanya wengine kuwa wanafunzi?
- Unafikiria nini kitatendeka ikiwa wafuasi wapya wataanza kushiriki na kufundisha wengine, mara moja?

## SOMA

**(Dakika 5)**

**Uwanafunzi wa Watoto wa Bata**

Karibu tena kwa mafundisho ya Zúme

Katika awamu hii, tutajifunza jinsi vifaranga wa bata wanavyojifunza kuelea kwa maji. Ni mbinu yakutufanya kuelewa kanuni mbili za kuanzisha uanafunzi.

Je umewahi kuona kundi la vifaranga wa bata wakitembea ?

Haijalishi popote ulipo duniani vifaranga wote wa bata siku zote wanafanana.

Mama wa vifaranga hao huwaongoza huku wanawe wakimfuata moja kwa moja kwa mpangilio. Mama hutangulia huku vifaranga hufuata nyuma taratibu.

Ila ukiangalia kwa makini na karibu , utaona kuna jambo linalotendeka. Kila kifaranga anashughulikia maswala mawili kwa wakati mmoja.

Kila kifaranga wa bata ni mfuasi, kwa sababu anafuata mwenendo wa mamake anatembea mbele yao. Na kwa wakati mmoja na uliokubalika.

Kila bata ni kiongozi, kwa sababu anaongoza huku vifaranga wakiwa nyuma yake.

Je bata ni mfuasi au kiongozi? Bata ni kiongozi na mfuasi.

Ni sababu tosha za bata akiwa anatembea ana majukumu yote ya kutengeneza wanafunzi.

Mungu anahitaji familia kukua kwa kiwango cha juu –na anatarajia kila mtu kuwa kiongozi, kila muumini kuwa mshiriki, na kila mwanafunzi kuandaa wanafunzi wengine kwa wakati mmoja.

Katika mtego mmoja tunaoangukia, kama mwanafunzi na anayetengeneza wanafunzi, ni imani potovu ambayo tunahitaji kujua kila kitu, au kila kitu, kabla hatujashiriki katika jambo lolote.

Ila hivyo sivyo uanafuzi hufanyika.

Wanafunzi ni kama vifaranga wa bata. Kuwa kiongozi, hawahitaji kujua kila kitu. Ilimradi wawe hatua moja mbele.

Mungu anahitaji familia yake kuwa waaminifu na anatarajia kila kiongozi kuwa mfuasi, kila anayeshiriki kuwa muumini, kila anayetengeneza wafuasi kuwa mwanafunzi kwa wakati mmoja.

Mtego mwingine tunaoangukia, kama mwanafunzi anayetengeneza wafuasi, nimafundishaye uongo ambayo mtu au mahali kila mmoja anajua ikiwa tutafuata baadaye itagundulika ni mtego.

Ila hiyo ni mbinu ya uanafunzi.

Katika ufalme wa Mungu tuna mama wa bata mmoja ambaye tunamfuata wote ni Yesu.

Hakuna mmishenari, wala mhubiri au profesa wa seminari ila Yesu tu ndiye anastahili kiwango cha imani yetu.

Yaliyosalia kwetu ni mchakato.

Kuna mmoja siku zote aliye karibu na Yesu ambaye twaweza kumfuata. Na kuna mmoja aliye mbali twaweza kumuongoza. Haijalishi nyadhifa zetu au roho zetu siku zote roho zetu zishikamane na Kristo.

Katika Bibilia Paulo aliyeandika mambo mengi katika agano jipya na aliyeanzisha makanisa mengi hakuandika “nifuate” anasema nifuate vile ninavyomfuata Kristo.

Paulo alijua kukuza kila mahali mnako wanafunzi walistahili kujua vile vile, kila kiongozi katika ufalme wa Mungu lazima awe mfuasi na wote tuamfuata Yesu.

Pia katika Bibilia Paulo anaandika:

“Kile umekisikia kutoka kwangu …waambie wengine kwa uaminifu, wale watakaowafundisha wengine pia.

Paulo alijua kuwa na wafuasi kila mahali na alijua kila kitu ambacho wanafunzi wanatakiwa kujua. Kila mfuasi katika ufalme wa Mungu sharti awe kiongozi na aongoze kama Yesu kutoa uhai kwa ajili ya wengine.

Ukihitaji kuona familia ya Mungu ikiongezeka kwa kasi na kwa uaminifu, fikiria kuhusu uanafunzi unaotengezwa kama bata kuwa mfuasi na kiongozi kwa wakati mmoja.

## JADILI

**(dakika 10)**

- Ni sehemu gani moja ya uanafunzi (kusoma / kuelewa Biblia, kuomba, kushiriki Hadithi ya Mungu, nk) ambayo unataka kujifunza zaidi kulihusu? Ni nani anayeweza kukusaidia kujifunza?
- Nini sehemu moja ya uanafunzi ambao unafikiri unaweza kushirikiana na wengine? Ungeliishiriki na nani?

## SOMA

**(Dakika 5)**

**Macho ya Kuona penye Ufalme Hauko**

Katika wamu hii tutajifunza jinsi ambapo ongezeko la uanafuzi hufanyika mbali na  kwa haraka wakati wanapoona ufalme wa Mungu hauko mbali.

Kama binadamu tunafikiria kuhusu kazi na vitu ambavyo tunavyona,Tunaviita vya ukweli. Vile vitu vilivyo .Ila ufalme unakua kwa kasi ikiwa tutazingatia kuona vitu visivyoonekana. Vitu ambavyo havipo. vitu ambavyo havipo

Kuna sehemu nyingi karibu nasi ambapo mapenzi ya Mungu hayajafanyika duniani kama vile mbinguni kuna mwanya mkubwa ambapo kuna kuvunjika kwa mioyo ,kusalitiana,machungu,dhiki na hata kifo vimekuwa mambo ya kawaida katika maisha ya kila siku.

Kila mwanafunzi-mfuasi wa Yesu anahitaji kuwa na uwezo wa kuona si tu sehemu ufalme wa Mungu ulipo ila mahali ufalme wa Mungu hauonekani.

Kazi ya ufalme wa Mungu ni kupenyeza sehemu ambazo kuna mianya ,sehemu za giza ili kuleta nuru katika sehemu hizo hasa tunamoishi katika ulimwengu huu.

Tunaweza kuona awamu mbili za ufalme wa Mungu ---kupitia watu tunaowajua na wale ambao huajakutana nao.

Kwanza kwa watu tunaowajua –katika mwendo wa mausiano ya marafiki na familia ,tunaofanya kazi nao,tunaosoma pamoja, majiriani na wengine wengi.

Hivi ndivyo hadithi ya Mungu inavyoenda kwa kasi sana. Tunawapenda na kuwajali sababu tayari tunawafahamu tayari. Ni kawaida.

Yesu alisimulia kisa cha tajiri aliyejipenda-mroho katika maisha na sasa alipata adhabu kuzimu. Tajiri anamsihi kwa kumtuma Lazaro Nenda kwa babangu awape onyo ndugu zangu watano ili wasije mahali hapa nilipo pa dhiki.

Yesu anatuonyesha jinsi walafi wanaoteseka wanao upendo kwa walio karibu nao.

Watu tunaowajua wamewekwa karibu nasi na Mungu ili tuonyeshe upendo wa Mungu na anahitaji tuwapende. Tunahitaji kuwa mawakili wema kwa uhusiano wa upendo na uvumilivu.

Wanafunzi wanaongezeka wakati wanajihisisha na watu wa Mungu waliokaribu nao na wana mipango ya kufanya jambo kuwahusu.

Unaweza kusaidia kwa kuwajali ili kutoa mchango wa kuwajenga na kutoa mpango wa kuongeza uzalishaji katika hatua chache.

Inafanyika hivi-Wafahamishe waandikwe watu 100 wanaowajua. Waambie sasa wagawe watu hao katika makundi matatu.

- Wale wanaomfuata Yesu
- Wale ambao hawamfuati Yesu.
- Wale ambao hawana uhakika ikiwa wanafuata Yesu au la.

Kwa wafuasi-wanafunzi wanaweza kuwatia moyo kwa kuongezeka na kuwa waaminifu.

Kwa wasioamini-wanafunzi wanaweza kujifunza jinsi ya kushirikiana nao na kuwasilisha katika upendo wa Mungu

Na kwa wale wasio na hakika-wanafunzi watajifunza jinsi ya kuwekeza kwa muda na kujifunza zaidi.

Kuna njia nyingine ambapo tunaona  ufalme wa Mungu haujafikiwa kwa watu ambapo hatujakutana nao.

Kuna watu wako nje ya mahusiano yetu-watu tusiowajua,majirani ambapo hatusemi nao zaidi ya neno ‘habari’ kwa wafanyabiashara wakiume au wakike tunakutana nao wanaopita katika barabara zetu, wageni vijijini, mji na jiji kamwe hatuwatembelei.

Yesu alisema-wafanye wanafunzi kote ulimwenguni.

Yesu alisema-utawaeleza kuhusu mimi kwanza Yerusalemu,Judea,Samariana ulimwenguni kote.

Kushiriki na watu unaowajua ni njia ambayo hadithi ya Mungu usambaa kwa haraka.

Kushiriki na watu usio wajua ni njia mojawapo neno la Mungu uenda mbali.

Ikiwa tunawapenda watu tusio wajua na kuwajali basi si kawaida ila ni nguvu za kiungu na ushahidi wa kazi ya Roho mtakatifu katika maisha yetu.

Wanaopendwa na Mungu ni wachache, wa mwisho na waliopotea. Hao ndio huwamwagia roho yake tena na tena.

Ikiwa tunahitaji kuwa kama Mungu,basi awa ndio tuahitaji kuwekeza katika maisha yetu.

Mungu ametuamrisha twende. Na sehemu ya kwenda ni kuenda na si wale walio karibu nasi bali wale walio katika giza nene la kiroho kwenye pembe zote za dunia hii-watu ambao hawawahi lisikia jina Yesu.

Neno la Mungu linasema-Mungu hapendi kiburi huwarehemu wanyenyekevu.

Kama wafuasi wa Yesu sharti tuwape wema vile anavyotupa-kuwa mnyenyekevu kwa wasio na uwezo na waliopotea.

Wanafunzi wanaongezeka wakati wanapojihusisha watu ambapo amewaka katika maisha yao.

Wanafunzi wanaongezeka hata zaidi wakati wanapojihusisha kwa watu wa Mungu ambapo hawapo karibu nao. Hata hivyo wanahitaji mpango wao.

Unaweza kusaidia kuongeza wanafunzi kwa kujali wengine ,kujenga mpango mdogo wa kutoa mafundisho kwa watu ambapo Mungu tayari ameandaa mioyo yao.

Yesu alisema-unapokaribia makazi sema “Mungu bariki nyumba hii na amani” Ikiwa watu wanaoishi humo ni wapenda amani basi maombi yako ya amani yatawabariki. Ila si wa amani, maombi yako yatakurudia.

Mwito kwa yeyote aliyeitwa tayari na Mungu aliyeandaliwa kusikiliza mtu wa amani-Aliyewajibishwa na ujumbe wa Mungu na mwaminifu kwa kutii na kushirikisha wengine.

Katika sehemu zingine tunajua machache badala ya kuwajali wengine kama marafiki,jamii, wafanyakazi wenzetu, tunaosoma pamoja nao, tunafundisha mtu jinsi atakavyo wafikia wenzake.

Matokeo mazuri siku zote huja wakati tunalenga waliowaaminifu. Kumbuka uaminifu utokana na kutii kile ambacho Mungu anatuambia na kuwapa wengine.

Watu waaminifu wanaotii na kuwapa wengine ni kama mchanga wa rutuba ambao Yesu anazungumzia kuhusu.

Yesu alisema-mbengu chache zilianguka kwenye udongo wa rutuba sehemu ambapo mimea huzaana mara thelathini au sitini ama mara mia moja vile zilivyo tawanyika.

- Watu wa Mungu hawana roho ngumu ya kukataa neno la Mungu.
- Waaminifu hawakati tama hata kama wanateswa au wakati kuwa mgumu.
- Watu waaminifu hawatatiziki kwa matatizo ya ulimwengu huu au utajiri usio dumu.
- Watu waaminifu ni kama wamepagawa sawa na yule mtu wa Gerasene aliyetii na kuwajulisha wengine kile Yesu alimuonyesha.

Mtu mwaminifu ni yule anayetii na kuwapa wengine papo hapo uzalisha wengi, wengi wanaotaka kumjua Yesu.

Tufungueni macho yetu tuone mahali ufalme haupo na kuzuru nje kupitia watu tunao wajua na watu tusio wajua na hivyo ndivyo wanafunzi wanaongezeka na ufalme wa Mungu unakuwa na kuenda kasi.

## JADILI

**(dakika 10)**

- Unajihisi vizuri kuishiriki na nani - - - watu ambao tayari unawafahamu au wale ambao hujawahi kukutana nao, bado?
- Unafikiri hiyo ni nini?
- Unaweza kuboreshaje kushiriki kwako na watu ambao hujihisi vyema nao?

## SOMA

**(Dakika 5)**

**Meza ya Bwana**

Yesu akasema- “Mimi ndimi mkate wa uzima ulioshuka kutoka mbinguni. Yeyote atakayeula mkate huu ataishi milele. Mkate huu ni mwili wangu, ambao nitatoa kuwa uzima kwa ulimwengu.”

Meza ya Bwana au “pasaka ya Bwana” ni njia mojawapo ya kusheherekea ukaribu wa muungano na uhusiano wetu na Yesu.

Hapa kuna njia ya kusheherekea-Wakati mnapokutana kama wafuasi wa Yesu,tumia muda kutafakari kimya,kwa utulivu zingatia na kutubu dhambi zako. Muelekeze mtu mmoja asome andiko hili.

Maana mimi nilipokea kwa Bwana yale maagizo niliyowaachieni: “Kwamba, usiku ule Bwana Yesu alisalitiwa, alitwaa mkate, akamshukuru Mungu, akaumega, akasema: "Huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa kunikumbuka." (1Wakorintho 11:23-24)

Pitisha mkate huo kwa kundi ambalo umelitenga ili wale.

Endeleza somo-- “Vivyo hivyo, baada ya kula, akatwaa kikombe akasema: "Hiki ni kikombe cha agano jipya linalothibitishwa kwa damu yangu. Fanyeni hivi, kila mnapokunywa, kwa kunikumbuka." (1Wakorintho 11:25)

gawa mvinyo au divai kwa kundi lako na kunywa mwenywe.

Maliza somo-- “Maana kila mnapokula mkate huu na kunywa kikombe hiki, mwatangaza kifo cha Bwana, mpaka atakapokuja.” (1Wakoritho 11:26)

Umeshiriki meza ya Bwana.

Sherehekea kwa kuomba na kuimba-wewe ni wake, naye ni wako!

Meza ya Bwana-Pasaka ya Bwana– sakramenti takatifu kutoka kanisa la kwanza na ni sehemu muhimu ya vifaa vya Zume.

## SHUGHULI

**(dakika 10)**

**Sherehekea Meza ya Bwana**

- Tumia dakika 10 zinazofuata kusherehekea Meza ya Bwana pamoja na kikundi chako.

**Maudhui:**

Unapokusanyika kama wafuasi wa Yesu:

1. Tumia muda katika kutafakari kwa utulivu, ukizingatia kimya kimya na kuungama dhambi zako.
2. Unapokuwa tayari, mwambie mtu asome kifungu hiki kutoka katika maandiko -- Kwa maana mimi nalipokea kwa Bwana niliyowapa ninyi, ya kwamba Bwana Yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mkate; na akiisha kushukuru, akaumega, akasema, Huu ni mwili wangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu. (1 Wakorintho 11:23-24)
3. Toeni mkate mliowatengea kundi lenu, mle.
4. Endelea kusoma -- Vivyo hivyo akakitwaa kikombe, baada ya kula, akisema, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi, kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu.' (1 Wakorintho 11:25)
5. Shiriki juisi au divai ambayo umetenga kwa ajili ya kikundi chako, na unywe.
6. Maliza kusoma: Kwa maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hicho, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo. (1 Wakorintho 11:26)

**Sherehekea kwa maombi au kuimba. Umeshiriki Meza ya Bwana. Wewe ni Wake, na Yeye ni wako!**

## ANGALIA

**(dakika 1)**

**Dhana zilizosikika katika kikao hiki:**

- Maono Kutupa Baraka Kubwa Zaidi
- Uwanafunzi wa Watoto wa Bata
- Macho ya Kuona penye Ufalme Hauko

**Zana zilizosikika katika kikao hiki:**

- Ushuhuda wa Dakika Tatu
- Meza ya Bwana

### HATUA IFUATAYO

## TII

Tumia muda wiki hii kufanya mazoezi ya Ushuhuda wako wa Dakika Tatu, na kisha ushiriki na angalau mtu mmoja kutoka kwenye Orodha yako ya 100 uliyoweka alama kuwa "Asiyeamini" au "Asiyejulikana."

## SHIRIKISHA

Uliza Mungu ambaye anataka umfundishe kwa zana ya Ushuhuda wa Dakika Tatu. Shiriki jina la mtu huyu na kikundi kabla hujaenda.

ZÚME

KIKAO CHA 5

## INGIA

**(dakika 1)**

Waruhusu washiriki wote na mwezeshaji waingie.

Au zume.training/checkin na utumie msimbo: **6542**

## OMBA

**(Dakika 5)**

Omba na kumshukuru Mungu kwa njia anazofanya kazi kupitia ushuhuda wa watu wake. Alika Roho wake Mtakatifu kuongoza wakati wako pamoja.

## ANGALIA NYUMA

**(Dakika 5)**

Kabla ya kuanza, chukua muda kutazama nyuma.

Mwishoni mwa kipindi kilichopita, kila mtu katika kikundi chako alipewa changamoto ya kufanya mazoezi uliyojifunza.

Chukua muda mfupi kuona jinsi kundi lako lilivyofanya juma hili.

## MAPITIO

**(dakika 1)**

**Katika kikao hiki, tutasikia na kujadili dhana hii:**

- Mtu wa amani

**Na tutaongeza zana hizi kwenye seti yetu ya zana:**

- B.L.E.S.S. Maombi
- Kutembea kwa Maombi

## SOMA

**(Dakika 5)**

**Kutembea kwa Maombi**

Neno la Mungu linasema kuwa lazima tuwe watu wa “maombi, wapatanishi na kutoa shukurani kwa watu wote,kwa wafalme na wale walio na mamlaka—ndipo tuishi kwa amani na maisha mazuri ya kiungu na utakatifu. Hivi ni vizuri,na inampendeza Mungu mwokozi wetu,anayetaka watu wote waokolewe na kuwa na maarifa ya ukweli.”

Kuomba ukitembea ni kifaa rahisi cha kutii amri za Mungu za kuombea wengine. Kuomba ukitembea ni vile inavyosikika-kuomba Mungu ukitembea hapa na pale.

Badala ya kufunga macho na kuinamisha vichwa, tunazidi kuzama na kuona vitu tunavihitaji vilivyo karibu nasi roho zetu zikinyenyekea kwa Mungu kuingilia kati.

Unaweza kuomba ukitembea kwa makundi madogo madogo ama unaweza kuomba ukitembea wewe mwenyewe.

Ikiwa utakuwa kwa kikundi-jaribu kila mmoja kuomba kwa sauti ya juu,kuzungumza na Mungu kuhusu kile anaona na anahitaji Mungu alete mioyoni mwao.

Kama uko peke yako-omba kimya kimya au kwasauti ya juu ikiwa unaomba na mtu mwingine umemkuta njiani.

Hapa kuna njia nne unaweza kujua kile unaomba wakati wa kuomba ukitembea.

- Kutazama—Unaona nini?Ikiwa unaona kibonzo cha mtoto kwenye bustani,unastahili kuombea watoto wa jirani,familia au shule za eneo hilo.

- Utafiti—Unajua nini? ikiwa umesoma kuhusu ujirani,unaweza kujua watu wanaoishi mahali hapo, au ikiwa eneo hilo linakumbwa na uhalifu au udhalimu. Ombea kuhusu vitu hivyo na muulize Mungu afanye jambo.
- Ufunuo-- Roho mtakatifu anaweza kukugusa roho yako au kukupa wazo kuhusu hitaji ama eneo la kuombea. Sikiliza-na uombe!
- Maandiko- Unaweza kusoma sehemu ya neno la Mungu kwa kujiandaa kwa kazi yake au ukiwa unatembea, Roho mtakatifu anaweza kukuletea andiko mawazoni. Ombea somo hilo na vile inaweza kuwa matokeo kwa watu wa eneo hilo.

Hapa kuna maeneo ya mvuto ambayo unaweza kuzingatia wakati wako wa maombi ya kutembea.

- Serikali-Tazama na uombee serikali hasa mahakama, majumba ya viongozi au ofisi za kutekeleza sheria. Ombea uimara wa maneno, mahali pa usalama, kwa haki na hekima ya uungu iwe kwa viongozi wetu.
- Biashara na maeneo ya kibiashara-ombea maeneo ya kibiashara mfano wa eneo lina biashara kwa wingi au maduka mengi. Ombea waekezaji na mawakili wema na wa vyanzo vyema. ombea uchumi wa haki na nafasi kutoa kwa moyo na Mungu anayetoa atawabariki anayewapa watu wake faida.
- Elimu-ombea vituo vya elimu kama shule majengo ya viongozi, vituo vya kufundisha, vyuo vya kijamii na vyuo vikuu. Ombea waalimu wenye haki ili wafundishe ukweli wa Mungu na kutunza mawazo ya wanafunzi. Omba Mungu aingilie kati kwa kila juhudi ili uongo na kuchanganyikiwa kusiwepo. Ombea sehemu hizo ili ziweze kutuma raia nje walio na nyoyo za kuhudumia na kuongoza.
- Mawasiliano- tafuta na uombee vituo vya mawasiliano kama vile redio, tevisheni na vituo vya kuchapisha magazeti. Ombea hadithi ya Mungu na ushuhuda wa wafuasi wake waweze kusambazwa katiki majiji na duniani nzima. Ombea ujumbe wake uenezwe kupitia vyombo vya habari kwa halaiki ya watu na kwa watu wa Mungu wataona kazi yake.
- Maswala ya kiroho-tafuta na uombee vituo vya kiroho kama vile majengo ya kanisa, misikiti au hekalu. Ombea kila anayetafuta maswala ya kiroho kupata amani na faraja kwa Yesu na si kuingiliwa au kukanganywa na uongo wa kidini.

Hatimaye, hapa kuna njia tano za kuomba wakati unapokuwa ukiomba ukitembea.

Unapotembea ukiomba, kuwa macho kwa nafasi na sikiliza roho wa Mungu ukiombea watu binafsi na makundi unaweza kukutana nao njiani.

Unaweza kusema. “Tunaombea jamii hii, kuna jambo tunaweza ombea?”

Ama sema “Naombea eneo hili, Je kuna jambo lolote ungetaka niombee?”

Baada ya kusikiliza jibu lao unaweza wauliza kuhusu mahitaji yao. Wakijishirikisha, waombee papo hapo. Ikiwa Mungu ataongoza, basi unaweza ombea maswala mengine tena.

Tumia neno bariki ili kukumbuka njia tano unaweza omba

- Mwili (afya)
- Kazi (kazi na fedha)
- Hisia (tabia)
- Jamii(mahusiano)
- Kiroho

Mara nyingi,watu huwa hufurahia unapowajali kwa kuwaombea.

Ikiwa mtu si mkristo,maombi yako yatafungua milango kwa mazungumzo ya kiroho na kupata nafasi ya kuzungumzia hadithi yako na ya Mungu. unaweza waalika kuwa miongoni mwa majadiliano ya Bibilia ama hata wakualike.

Ikiwa mtu ni mkristo unaweza kuwaalika kujiunga na maombi ya kutembea wafundishe watakavyo omba wakitembea na kuombea maeneo yaliyo na mvuto, ama maombi ya baraka ili famila ya Mungu ikue zaidi.

Maombi ya kutembea-ni chombo rahisi sana katika kitabu cha Zume.

---

## SOMA

**(Dakika 5)**

**Mtu wa amani**

Karibuni tena kwa mafundisho ya Zúme.

Katika kikao cha awali tulijulishwa kwa wazo la mtu wa Amani. Katika kikao hiki tutaingia kwa undani zaidi kuona huyu mtu anaweza kuwa nani na jinsi ya kufahamu ikiwa umepata mmoja. Mtu wa amani kwa haraka anaweza kusaidia kuzalisha wanafunzi – hata mahali ambapo wanafunzi wa Yesu ni wachache na wako mbali mbali.

Wakati Yesu alipotuma wafuasi wake katika maeneo mapya ili kuwafanya wanafunzi, aliwapa amri rahisi lakini yenye maarifa.

Yesu alisema - - Wasichukue pesa za bindoni, wala mkoba, wala viatu; wasisalimie mtu njiani. Nyumba yoyote waingiapo, kwanza semeni, 'Amani na iwe ndani ya nyumba hii.' Kukiwemo na mtu wa amani mle ndani, amani yenu itakaa juu yake; kama sivyo, itawarudieni. Kaeni humo, mkila na kunywa watachowapa; kwa kuwa mfanyakazi anastahili ujira wake. Msiende nyumba hadi nyumba.

Lakini hiyo yote inamaanisha nini?

Wakati tunapofikiria kuwafanya wanafunzi, mawazo yetu kwanza yatakuwa – tuwe na pesa za kutosha, tuchague lengo dhahiri, na tuwe na mpango dhahiri wa utekelezaji. Ikiwa Yesu alisema - “NENDA,” sharti “tuende” na tuzidi kuenda! Ambia kila mtu! Kila mahali! Kila wakati!!!

Lakini Yesu, katika amri yake, hakuonekana kuwa na wasiwasi juu ya fedha na juhudi, na kujihusisha sana na alilolenga.

Yesu alitaka wafuasi wake kuangalia – na kuwekeza – kwa mtu wa amani.

Ikiwa unataka kufanya wanafunzi mahali ambao sio wengi – au pengine hata – wapo, hapo kumpata mtu wa Amani ni kitu cha maana unaweza kufanya.

Mtu wa Amani ni:

- Mtu ambaye yuko WAZI kusikia Hadithi yako,Hadithi ya Mungu na Habari Njema ya Yesu.
- Mtu ambaye ni MKARIMU na ANAKUKARIBISHA nyumbani kwake au mahali pa kazi au kujiunga na jamaa na marafiki katika jambo.
- Mtu ambaye ANAJUA WENGINE (au ANAJULIKANA NA WENGI) na mwenye furaha kuunganisha kundi ndogo au umati.
- Mtu ambaye ni MWAMINIFU na HUSHIKIRIKIANA yale aliyojifunza na wengine – hata baada ya wewe kuwaacha.

Katika Biblia, tunajifunza kwamba Yesu na wafuasi wake walikutana na Watu wa Amani - ghafla.

Katika nchi ya Wagerasi, Yesu alikutana na mtu mwenye pepo na aliishi peke yake akiwa amefungwa minyororo. Hatuwezi kumdhania kuwa Mtu wa Amani, lakini alikubali kumsikiza Yesu. Alikuwa MKARIMU na hata KUMKARIBISHA Yesu kule alikuwa anaishi. Alikuwa anajulikana vizuri na angeweza kuvutia umati kwa urahisi – hata kama tabia yake ni mbaya.

Na Yesu aliona kwamba yeye ni MWAMINIFU na hapo AKASHIRIKI naye pamoja na jamaa yake jamii yake na nchi yake yote kile Yesu anamaanisha kwake. Kwa kweli, wakati Yesu aliporudi pale katika eneo

lile, umati mkubwa ulijikusanya, wakiwa na furaha ya kuona Mtu ambaye wamesikia mambo mengi kumhusu.

Kule Samaria, Yesu alikutana na mwanamke kisimani. Akawa wazi kwa Yesu, kwa nia ya kuwa MKARIMU na kujibu ombi lake la kunywa maji. Tunajifunza kwamba alikuwa na waume watano na bado alikuwa anaishi na mume mwingine, na kwa hivyo katika mji huu mdogo, alikuwa na hakika kwamba ANAJULIKANA KWA WATU WENGINE. Na Yesu akaongea naye, alikuwa MWAMINIFU na AKASHIRIKIANA – kwa haraka ambapo hata mji mzima ukamuomba Yesu abaki pale akashiriki nao, pia. Alikubali.

Kwa hivyo, ikiwa Mtu wa Amani anaweza kuishi mahali popote, na kufanya chochote, na kuwa mtu ambaye tunamjua au tunakutana naye – tunawezaje kupata mmoja?

Hapa kuna njia tatu rahisi - -

Tunaomba mapendekezo kutoka kwa watu katika jamii – Ni nani anayeaminika hapa? Je, kuna mtu hapa ambaye anafikiria watu wengine kwanza kabla ya kujifikiria? Ikiwa tutasikia jina hilo tena na tena – tutajaribu kukutana naye, kushirikiana wazo la kiroho, na kuona ikiwa wako tayari kusikia na kushiriki.

TUNAJITOA kuombea mtu wakati tunafanya Maombi ya Kutembea, au kazini, au michezoni – wakati wowote panapo fursa – na kisha kubadilisha maombi hayo kuwa mazungumzo ya kiroho.

TUNAINGIZA mawazo ya kiroho katika mazungumzo ili kuona ikiwa Mungu anateda katika maisha ya mtu. Ikiwa wako tayari na wenye nia, basi tunauliza ikiwa wanaweza kukusanya kikundi kujadiliana hata mengi.

Uliza mapendekezo, KUJITOLEA kuomba, INGIZA mawazo ya kiroho. Hizi zote ni njia ambapo tunaweza kuanzisha mchakato wa kupata Mtu wa Amani. Na haijalishi tunawapataje, kumbuka Yesu alisema tunastahili kutumia wakati mwingi wa kufanya wanafunzi na Mtu wa Amani.

Ni rahisi kufikiria kwamba ni “haki” kutumia wakati mchache kwa kila mtu, kwa usawa. Lakini Yesu alisema – na kuonyesha – hataki tuwe watu wa ki juju kwa kila mtu bali kupeana kwa undani kwa wachache.

Yesu mara nyingi alivutia umati, lakini Biblia inatuambia tena na tena kwamba Yesu angelijitenga kutoka kwa umati na kutumia wakati wake na wafuasi wake wa karibu kumi na wawili.

Mara kadhaa, Yesu angetumia wakati mwingi na kundi dogo la watu watatu peke.

Ikiwa Yesu, ambaye alikuwa na uwezo zaidi, nguvu nyingi, mamlaka zaidi, nidhamu, hekima, maarifa,  kuelewa na huruma alichagua kutumia wakati akiwekeza kwa wachache na kuambia wafuasi wake nao wafanye vivyo hivyo, je, si ni ya muhimu tunapaswa kufuata na kushirikiana kwa mfano wake mkamilifu?

Mtu wa Amani

Sio rahisi kuzipata – huenda ni moja kwa elefu. Lakini kama hazina iliyofichwa inayostahili kutafutwa, thamani yao ya kukuza jamaa ya Mungu haipimiki.

## JADILI

**(dakika 10)**

- Je! Mtu mwenye "sifa mbaya" (kama mwanamke Msamaria au mtu aliyekuwa na pepo huko Garasi) anaweza kuwa Mtu wa Amani? Kwa nini au kwa nini sivyo?
- Je! ni jumuiya au sehemu gani ya jamii iliyo karibu nawe inayoonekana kuwa na uwepo mdogo (au hakuna) wa Ufalme?
- Je, Mtu wa Amani (mtu ALIYE WAZI, MKARIMU, ANAWAJUA WENGINE na ANASHIRIKI) angewezaje kuharakisha kuenea kwa Injili katika jumuiya hiyo?

## SHUGHULI

**(dakika 10)**

**Fanya mazoezi ya B.L.E.S.S. Maombi**

- Gawa katika vikundi vya wawili au watatu na ujizoeze kusali maeneo matano ya B.L.E.S.S. Sala juu ya kila mmoja.

**Maudhui:**

**Mfumo wa maombi ya BARAKA**

Mfumo wa maombi ya BARAKA unatoa njia tano unazoweza kuwaombea watu unaokutana nao wakati wowote, lakini hasa unapotembea katika maombi.

- Mwili - afya
- Kazi - kazi na fedha
- Kihisia - ari

- Mahusiano ya kijamii
- Kiroho - kumjua na kumpenda Mungu zaidi

## SHUGHULI

**(Dakika 60 - 90)**

**Kutembea kwa Maombi**

- Mkajigawanye kwa vikundi vya watu wwili au watatu na mkaende kwa jamii kujizoeza Maombi ya Kutembea.
- Kuchagua eneo inaweza kuwa rahisi kama kutembea nje kutoka mahali ambapo ulipo sasa, au unaweza kupanga mpango kwenda mahali pemgine maalum.
- Nenda jinsi Mungu anavyokuongoza, na upange kutumia dakika 60-90 kwa shughuli hii.
- Kipindi hiki kinaisha na shughuli ya kutembea kwa maombi.

**Maudhui:**

**Vyanzo vinne vinavyoweza kuongoza maombi yako:**

1. ANGALIZO Unaona nini? Ukiona kichezeo cha mtoto kwenye uwanja, unaweza kuchochewa kuombea watoto wa ujirani, familia au shule katika eneo hilo.
2. UTAFITI Je! Unajua nini? Ikiwa umesoma kuhusu ujirani, unaweza kujua jambo fulani kuhusu watu wanaoishi huko, au ikiwa eneo hilo linakabiliwa na uhalifu au ukosefu wa haki. Omba juu ya mambo haya na umwombe Mungu atende.
3. UFUNUO Roho Mtakatifu anaweza kuugusa moyo wako au kuleta wazo akilini kwa ajili ya hitaji fulani au eneo fulani la maombi. Sikiliza - na uombe!
4. MAANDIKO Huenda umesoma sehemu ya Neno la Mungu katika kujitayarisha kwa ajili ya kutembea kwako au unapotembea, Roho Mtakatifu anaweza kukukumbusha Maandiko. Omba kuhusu kifungu hicho na jinsi kinavyoweza kuwaathiri watu katika eneo hilo.

**Maeneo matano ya ushawishi ya kuzingatia maombi:**

1. SERIKALI Tafuta na kuombea vituo vya serikali kama vile mahakama, majengo ya tume au ofisi za utekelezaji wa sheria. Ombea ulinzi wa eneo hilo, haki na hekima ya kimungu kwa viongozi wake.

2. BIASHARA NA BIASHARA Tafuta na uombee vituo vya biashara kama vile wilaya za kifedha au eneo la ununuzi. Ombea uwekezaji wa haki na uwakili mzuri wa rasilimali. Ombea haki ya kiuchumi na fursa na watoaji wakarimu na wacha Mungu wanaotanguliza watu mbele ya faida.
3. ELIMU Tafuta na uombee vituo vya elimu kama vile shule na majengo ya utawala, vituo vya mafunzo ya ufundi stadi, vyuo vya jamii na vyuo vikuu. Sali ili waelimishaji waadilifu wafundishe kweli ya Mungu na kulinda akili za wanafunzi wao. Omba kwamba Mungu aingilie kati katika kila juhudi kuendeleza uwongo au machafuko. Omba kwamba maeneo haya yatume raia wenye busara ambao wana moyo wa kutumikia na kuongoza.
4. MAWASILIANO Tafuta na uombee vituo vya mawasiliano kama vile vituo vya redio, vituo vya televisheni na wachapishaji wa magazeti. Ombea Hadithi ya Mungu na ushuhuda wa wafuasi Wake kuenea katika jiji zima na duniani kote. Omba kwamba ujumbe Wake utolewe kwa njia Yake kwa umati Wake na kwamba watu wa Mungu kila mahali waone kazi ya Mungu.
5. UROHO Tafuta na uombee vituo vya kiroho kama vile majengo ya makanisa, misikiti au mahekalu. Omba kwamba kila mtafutaji wa kiroho apate amani na faraja katika Yesu na asikengeushwe au kuchanganyikiwa na dini yoyote ya uwongo.

## OMBA

**(Dakika 5)**

Kabla hujatoka kwenye shughuli yako ya Kutembea kwa Maombi, hakikisha unaomba pamoja na kikundi chako ili kumaliza muda wako pamoja.

Asante Mungu kwa kuwa anawapenda waliopotea, wa mwisho na wa mwisho - tukiwemo sisi!

Mwambie auandae moyo wako na moyo wa wale utakaokutana nao wakati wa matembezi yako kuwa wazi kwa kazi Yake.

ZÚME

KIKAO CHA 6

## INGIA

**(dakika 1)**

Waruhusu washiriki wote na mwezeshaji waingie.

Au zume.training/checkin na utumie msimbo: **1235**

## OMBA

**(Dakika 5)**

Omba na kumshukuru Mungu kwa yale aliyofanya katika kipindi kilichopita, mwombe akusaidie unapoona ni vigumu kutii, na umkaribishe Roho wake Mtakatifu kuongoza wakati wako pamoja.

## ANGALIA NYUMA

**(Dakika 5)**

Kabla ya kuanza, chukua muda kutazama nyuma.

Mwishoni mwa kipindi kilichopita, kila mtu katika kikundi chako alipewa changamoto ya kufanya mazoezi uliyojifunza.

Chukua muda mfupi kuona jinsi kundi lako lilivyofanya juma hili.

## MAPITIO

**(dakika 1)**

**Katika kikao hiki, tutasikia na kujadili dhana hii:**

- Uaminifu ni bora kuliko Ujuzi

**Na tutaongeza zana hii kwenye seti yetu ya zana:**

- 3/3 Mkutano wa Kikundi

## SOMA

**(Dakika 5)**

**Uaminifu**

Katika kikao hiki, tutajifunza jinsi UAMINIFU ni kipimo bora cha ukuaji wa kiroho kuliko maarifa na mafundisho. Kuna mawazo mawili ambayo yamesababisha matatizo kadhaa kanisani, leo.

Kwanza ni kwamba wazo la ukuaji wa kiroho wa mtu umeunganishwa na jinsi unavyolielewa neno la Mungu. Wao hufanya kana kwamba ni IMANI YA HAKI – au imani halisi – ni kipimo kizuri cha imani ya mtu.

La pili ni kwamba wazo la uwezo wa mtu wa kuongoza unahitaji "mafundisho kamili" kabla waanze kuhudumia. Wao hufanya kana kwamba MAARIFA KAMILI – nicho kipimo cha uwezo wa mtu wa kuhudumu.

Shida na wazo la kwanza – ni kuegemea – IMANI KAMILI – au "imani ya haki" ni kwamba Shetani, mwenyewe, anaelewa maandiko kuliko mwanadamu yeyote. NENO la MUNGU linasema – unaamini kwamba kuna Mungu mmoja. Sawa! Hata mapepo wanaamini hivyo – na kutetemeka.

Kipimo kizuri cha ukuaji wa kiroho wa mtu ni  IMANI ZOEFU - "zoezi la haki".

Tunapaswa kujihusisha sana na UAMINIFU katika KUTII na KUSHIRIKIANA kuliko kupima ukuaji wa kiroho kwa yale tunayoyajua pekee.

Shida na wazo la pili – ya kwamba mtu lazima awe amesoma zaidi kabla wawe viongozi  kwamba hakuna aliyefundishwa zaidi.

Yesu alituma viongozi wachanga ambao bado wana mengi ya kujifunza ili waweze kufanya kazi zingine muhimu katika Ufalme.

Neno la Mungu linasema – Yesu aliwaita wafuasi wake wote kumi na wawili na akawapa uwezo juu ya mapepo wote na magonjwa. Kisha akawatuma kutangaza kuhusu Ufalme wa Mungu na kuwaponya wagonjwa.

Watu hawa walitumwa kabla Petro kushiriki imani yake kwamba Yesu ni Mwokozi – kitu kile tunachukulia kama hatua ya kwanza ya imani. Na hata baada ya kutumwa Yesu bado alimkemea Petro mara kadhaa kwa makosa na Petro baadaye bado alimkana Yesu. Wafuasi wengine walibishania uongozi kati yao na kazi ya kila mmoja katika Ufalme wa Mungu ujao.Wote walikuwa na mengi ya kujifunza, lakini Yesu aliwaweka wote kufanyanya kazi, kushirikia mtu walichojua tayari.

Uaminifu – ni zaidi mafundisho – ni kitu ambacho kinchoweza kuanzishwa unapoanaza kumfuata Yesu.

Uaminifu – Zaidi ya mafundisho.

Ikiwa TUNATII na KUSHIRIKIANA na wengine yale tumesikia, sisi ni waaminifu.

Ikiwa tutasikia na TUKATAE kutii na kushirikiana, sisi si waamini.

Tunapozidisha wanafunzi, hebu na tuhakikishe kwamba tunapima vitu vilivyo sahihi.

## JADILI

**(dakika 10)**

Fikiria juu ya amri za Mungu ambazo tayari unazijua. Je, wewe ni "mwaminifu" kiasi kipi wa kuitii na kushiriki mambo hayo?

## SOMA

**(dakika 75)**

**3/3 Mkutano wa Kikundi**

Karibu tena kwa mafundisho ya Zumé. Katika kipindi hiki tutajifunza jinsi thelusthi 3/3 (FAHAMU: TAMUKA HIVI “Theluthi-Tatu”) Kikundi ni njia ya kukutana kinachowasaidia wafuasi wa lYesu kuweza kusaidiana wenyewe esnspomfuata Yesu kwa karibu.

Yesu alisema - - “kwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo paop hapo katikati yao.” Hiyo ni ahadi yenye nguvu, na ambacho kila mfuasi wa Yesu anastahili kuiona kama faida. Lakini mnapokutana kama kundi, Je, mnatumiaje wakati wenu?

Theluthi 3/3 Kundi kile ambacho hugawanyisha wakati wao pamoja katika sehemu tatu ili waweze kujizoeza kutii baadhi ya mambo muhimu yanayoamurishwa na Yesu.

Inatumika hivi:

- **Theluthi tatu** ya kwanza ya kundi kinatumika kwa kuangalia yale yaliotendeka tangia tuwe pamoja.
- **Theluthi ya kati** ya kundi kinatumika kwa Kuangalia Hekima ya Mungu na mwelekeo wake katika maandiko, majadilianao na maombi.
- **Theluthi ya mwisho** ya wakati wa kundi hutumika kwa Kuangalia mbele jinsi tunavyoweza kutumia na kutii yale tumejifunza.

Katika kikao hiki kundi lako litaongozwa kupitia toleo fupi la theluthi tatu la kundi kuwasaidia kujitayarisha kwa masimulizi kamili katika maisha halisi.

Kumbuka kikao kwa kupumua kiroho? Vuta hewa ndani, sikia kutoka kwa Mungu. Achilia hewa itoke, tii yale unayoyasikia na ushirikishe wengine. Hicho ndicho theluthi 3/3 hasa.

Kundi la theluthi 3/3 ni kile ambacho kinagawanyisha wakati wake katika sehemu tatu, ili waweze kujizoeza kusikia kutoka kwa Mungu na kutii na kushirikiana baadhi ya mambo muhimu yanayoamurishwa na Yesu.

Kikao hiki chafaa kudumu lisaa limoja, na litaenea kwa haraka. Ukiwa na kikundi kikubwa ama kikundi kipendacho majadiliano ya kindani, unaweza ukauliza mmoja wa kikundi asaidie kuweka wakati kwa kutumia saa.

Kwa Maisha halisi, hatua hizi zitaenea pole pole, lakini unapo fanyia mazoezi hakikisha unazidi kuendelea ndiposa usiishiwe na saa. Usiruke hatua zozote – zote ni muhimu!

Kumbuka kwamba kundi la theluthi 3/3 si sawa na Masomo ya Biblia – hiyo ni kwa kusudi! Tumia uzoefu huu kama fursa ya kujifunza njia mpya ya kukutana na yale yote mazuri Mungu amepangia wakati wenu mkiwa pamoja.

Mko tayari? Na tuanza!

**KUTAZAMA NYUMA**

Muda yetu ya kwanza ya theluthi ya kwanza tutaitumia kwa kuangalia nyuma kwa kujaliana na kutoa shukrani, kwa kushikiana mapambano yetu na kuombea wanachama wengine wa kundi letu. Tutaangalia kuona ikiwa kila mtu katika kundi amepata fursaya kutii na kushiriki pamoja na wengine yale waliyojifunza wakati wa mwisho tuliokuwa pamoja.

**Hatua ya Kwanza - "Kutoa Shukrani."**

Mpa kila mtu muda wa kushiriki na wengine chochote anatoa shukrani kwalo. Bonyeza kidude cha video cha kusimamisha na ufanye hivyo sasa hivi...Je, bado uko pale? Kweli, tunataka ubonyeze kidude cha kusimamisha, ili kila mmoja katika kundi lako aweze kushiriki na wengine kile anachomshukuru Mungu kwalo. Tutakuwa papa hapa mkirejea.

**Hatua ya Pili - "Kushiriki Jitihadi zako" and "na Kuombeana."**

Hebu sasa kila mtu katika kundi lako ashiriki na wengine kile wachopambana nalo. Mtu mwingine anaweza kuombea yale wanayoyashiriki na wengine. Bonyeza kidude cha kusimamisha, kisha shiriki na uombe.

**Hatua ya Tatu - "Kuzingatia Kundi."**

Kila wakati mkutanapo, mnastahili kuchukua wakati wenu kufikiria ni kwa nini muko pamoja – kumpenda Mungu, kuwapenda wengine, kumshiriki Yesu, na kuwasaidia wengine kumshiriki pia pia.

Kunazo njia nyingi ambazo kundi linaweza kuzinatia katika huduma, lakini katika kikao hiki cha mazoezi acha mtu asome kwa sauti Mathayo 22:37-38. Bonyeza kidude cha kusimamisha, kisha asome.

**Hatua ya Nne - "Kuthibitisha."**

Hii ni sehemu ambayo baadhi ya makundi wanataka kuruka kwa sababu inamaanisha kuuliza maswali ambayo wakati mwingine inaweza kuwa ngumu.

Tafadhali usiiruke.

Yesu aliwapenda wafuasi wake hata kuwauliza maswali magumu. Ikiwa tunataka kuwa kama Yesu, tuwapende wengine hata kuweza kufanya vile. Katika hatua hii, mtu mmoja katika kundi anapeana ripoti kuhusu ikiwa alitii yale alisikia Mungu akimweleza kufanya wakati wa mwisho mlipokuwa pamoja.

Katika kila kipindi cha Zume, tumeweka ahadi hizi katika hatua yetu ya kuangalia mbele ambapo tunakuomba uitii, mkaishiriki na muombe. Tumeweka kielelezo cha uajibikaji ya hatua ya kuangalia nyuma ambapo tunakuomba Ukaangalie ahadi hizo.

Ikiwa hamkuwa mnatumia muda mwingi kwenye hatua hizi hadi sasa katika mafundisho, huu ni wakati mzuri wa kuanza.

Sehemu ya kumpenda Mungu na kutii anachotuambia. Sehemu ya kupendana ina maana kumsaidia mtu kutii wanachosikia kutoka kwa Mungu.

Upendo inamaanisha kuchukulia ahadi za mtu kwa uzito – na kuwaonyesha upendo kwa neema – wote kwa wakati moja.

Bonyeza kidude cha kusimamisha na ambia  kila mtu ajibu maswali yafuatayo?

- Je, umetii aje yale umejifunza hadi sasa?
- Umefundisha nani yale umejifunza?
- Umeshiriki na nani hadithi yako ama hadithi ya Mungu tangu tuwe pamoja kama kikundi?

Tunapomalizia sehemu ya kutazama nyuma ya kundi letu la theluthi 3/3, hapa kuna kitu cha kusaidia vikao vyenu kuboreka zaidi:

**KIDOKEZO CHA MAFUNDISHO YA ZUME**

Wakati mwingine katika kundi, mtu mmoja anaweza kuwa ndiye mnenaji kila wakati. Hili lisitendeke. Kila mtu katika kundi ako na thamani, kwa hivyo hakikisha kwamba kila mmoja anapata nafasi ya kushirki.

Ikiwa wengine hawapati nafasi ya kuongea, basi kwa upole elezea yule anayenena zaidi kwamba kila mtu anapaswa kusikizwa.

**KUTAZAMA JUU**

Katikati ya wakati ya theluthi tatu yetu pamoja, tunamkaribisha Roho Mtakatifu wa Mungu kutuongoza kuelewa vyema Neno la Mungu.

Kwa sauti ya juu tutasoma fungu kutoka kwenye Biblia kisha tuulize na kujibu maswali rahisi kama kundi kutusaidia kuchunguza na kuelewa vizuri malengo na mipango ya Mungu.

**Hatua ya Kwanza – Mkaribishe Roho Mtakatifu wa Mungu Aongoze**

Chukua muda mfupi ili uombe. Ongea na Mungu kwa urahisi na kwa ufupi. Omba Roho wake Mtakatifu akufundishe kutoka kwenye kifungu ambacho unaenda kukisoma. Bonyeza kidude cha kusimamisha kisha omba.

**Hatua ya Pili – Soma Neno la Mungu na Ukaulize Maswali**

Mtu mmoja katika kundi asome kutoka kwenye Biblia. Kwenye kikao hiki cha mazoezi, soma Luka 18:9-14. Akishamaliza kusoma, kundi linapaswa kujibu maswali mawili:

- Ulipenda nini kuhusu kifungu hiki?
- Changamoto ilikuwa nini ama kilichokuwa kigumu kuelewa?

Ikiwa kunao wanafuzi – watu ambao hawasomi vizuri ama wanaopenda kujifunza kwa kusikia – katika kundi lenu, hakikisha umesoma kifungu angalau mara mbili.

Bonyeza kidude cha kusimamisha, soma na ujibu maswali.

Sasa acha mtu mwingine akasome kifungu hicho mara ya pili, kisha kundi lijibu maswali haya mawili:

- Je, unaweza kujifunza kuhusu watu katika kifungu hiki?
- Je, tunaweza kujifunza nini kumhusu Mungu kutoka kifungu hiki?

Kumbuka kuzingatia kifungu kwa njia rahisi!

Hiyo ndio mwisho ya sehemu ya Kutazama Juu ya theluthi 3/3 yetu, na hapa kuna kitu cha kusaidia vikao vyenu kuwa hata bora zaidi:

**KIDOKEZO CHA MAFUNDISHO CHA ZUME**

Wakati unapojifunza Kumbuka kukaa katika vifungu vya Neno la Mungu, zingatia maneno yake badala ya vitabu vingine, walimu, au maoni. Badala ya kuuliza, “Unafikiri hii inamaanisha nini?” uliza “Kifungu hiki kinasema nini?”

Ikiwa kuna mtu katika kundi lenu ambaye angependa kufundisha, kwa upole mkumbushe kwamba Roho Mtakatifu wa Mungu na neno kamili linaweza kufundisha kundi. Sote tuko hapa kwa minajili ya kufifunza, pamoja. Na usiogope ukimya ama kusimamishwa kiasi kwa majadiliano. Mungu anafanya kazi hata kukiwa kimya.

Endelea kilenga Neno Lake, baki kwa kifungu, mtumainie Mungu kutenda mengine.

**KUANGALIA MBELE**

Katika theluthi tatu ya mwisho ya wakati wetu, tunazingatia kuangalia mbele jinsi tunavyoweza kutii na kuwafundisha wengine yale tumejifunza kutoka kwa neno la Mungu.

Kila mwanachama wa kikundi anauliza Mungu maswali machache rahisi kisha anaongojea majibu yake kwa maombi. Kisha tunashiriki na kutekeleza ahadi zetu na kuomba kumaliza wakati, wetu pamoja.

**Hatua ya 1 – Kuombea kusudi lake Mungu**

Kila mmoja katika kundi lenu aombe kimya na amwulize Mungu maswali haya:

Mungu, naweza kutii na kumiaje yale unanifundisha?

- Naweza kufundisha akina nani kutokana na kifungu hii ili waweze kujifunza na kukupenda zaidi?

- Je, ungependa nishiriki na nani ushuhuda wangu au Habari njema za Yesu?

Bonyeza kidude cha kusimaisha kisha ukaombe.

Omba Roho Mtakatifu wa Mungu akupe majibu maalum, majina maalum na hatua maalum ambazo unaweza kuchukua wakati huu na wakati kundi lenu litakapo kutana tena.

**Hatua ya 2 – Kukusanya ahadi**

Uliza kila mtu katika kundi lako kushiriki na wengine yale waliyoyasikia kutoka kwa Bwana kwa kila swali. Huenda mtu hakusikia lolote kutoka kwa Bwana kwa swali moja, mbili, au hata zote tatu. Wanaweza tu kutoa ripoti kwamba hawakusikia lolote.

Lakini kumbukeni, kundi lazima lisikie kutoka kwa Bwana. Yesu alisema - “Kondoo wangu husikia sauti yangu.” Na hatua zako za utiifu zilivyo, itakuwa rahisi kuzitii kabla tukutane tena.

Bonyeza kidude cha kusimamisha, kisha shiriki na wengine yale uliyoyasikia.

**Shatua ya 3 – Kujizoeza na mpango wako**

Kabla muda wenu pamoja kuisha, gawanyeni kundi lenu la theluthi 3/3 kwa vikundi viwili ama vitatu vidogo vidogo na mjaribu kufanya yale mmesikia Bwana anawaeleza mkafanye.

Kumbukeni – kujizoeza sio kutii, kujifundisha ama kushiriki, bali inawatayarisha kuwa tayari kufanya mambo hayo vizuri sana.

Kila kundi ndogo likamilishe zoezi lake kwa maombi.  Ombea hao watu hasa na mipango Mungu ameweka ndani ya mioyo yenu.

Ikiwa muko na wanafunzi wasioweza kuandika katika kundi lenu, tenga wakati wa kuwasomea tena vifungu vya neno la Mungu mliosoma awali.Hili litasaidia kundi lote kuwa tayari kushiriki na wengine watakaokutana nao katika mikutano.

Bonyeza kidude cha kusimamisha, kisha mjigawanye katika vikundi kujizoeza na kuomba. Mtu yeyote asiyekuwa na shughuli maalum na ajizoeze kushiriki hadithi ya ushuhuda wake au hadithi ya Mungu.

Unapoleta kundi lako pamoja tena, chukua muda wako kusherehekea! Sasa mmekamilisha sehemu ya Kuangalia Mbele na mmejizoeza theluthi 3/3  ya muundo wa kikundi.

Kundi litaendelea kujizoeza bila mwongozo huu wa video katika vikoa vya baadaye. Hakikisha mnabadilishana ili wengine nao waongoze mchakato. Sio lazima uwe mwalimu mwenye ujuzi, fuata tu hatua hizi rahisi.

Kabla hamjaondoka, hapa kuna kidokezo kimoja cha kusaidia vikao vyenu kuwa hata bora zaidi:

**KIDOKEZO CHA MAFUNDISHO CHA ZUME**

Kote duniani, makundi ya theluthi 3/3 huwa wanashiriki meza ya Bwana pamoja, au chakula na mazungumzo ya kawaida kama sehemu ya wakati wao pamoja.

Mungu alitupa ushirika kama huu - - kujifunza kwa maksudi na kukua na kuishi kwa maksudi na uhusiano kusaidia kutupa nguvu, kutuhimiza, na kutujenga ili tuwe kama Mwanawe, Yesu.

Na ni hivyo – kundi lako sasa limejizoeza sehemu zote tatu – Tunaangalia nyuma kuhakikisha yale tumetimiza tangia wakati wa mwisho tulipokutana, Kuangalia Juu ili kuelewa  yale Mungu anavyo kwetu kujifunza pamoja katika wakati huu, na tunaangalia Mbele kuweka vitedo vyote ambavyo Mungu ameweka ndani ya mioyo yetu wakati tulikuwa mbali mbali.

Kikundi cha theluthi 3/3 -  njia rahisi ya kukutana inayotusaidia kuwa kama Yesu.

## JADILI

**(dakika 10)**

- Je, umeona tofauti yoyote kati ya Kundi la 3/3 na Masomo ya Biblia au Kundi ndogo ambayo umekuwa sehemu yake (au umewahi kusikia) katika siku za nyuma? Ikiwa ndivyo, utofauti hizo zinaathiri kundi hizo kiaje?
- Je, Kundi la 3/3 linaweza kuchukuliwa kuwa Kanisa Rahisi? Kwa nini au kwa nini?

## ANGALIA

**(dakika 1)**

**Dhana zilizosikika katika kikao hiki:**

- Uaminifu ni bora kuliko Ujuzi

**Zana zilizosikika katika kikao hiki:**

- 3/3 Mkutano wa Kikundi

**HATUA IFUATAYO**

## TII

Tumia muda wako juma hili kutii, mafunzo, na kushirikiana kulingana na ahadi ulizofanya wakati wa mazoezi ya Kundi la 3/3.

## SHIRIKISHA

Omba na umuulize Mungu yule anataka ushiriki naye muundo wa Kundi 3/3 kabla kundi kukutana tena. Shiriki jina la mtu huyu na kundi kabla ya kwenda.

ZÚME

KIKAO CHA 7

## INGIA

**(dakika 1)**

Waruhusu washiriki wote na mwezeshaji waingie.

Au zume.training/checkin na utumie msimbo: **4322**

## OMBA

**(Dakika 5)**

Omba na kumshukuru Mungu kwa kujitolea kwa kikundi kumfuata Yesu kwa uaminifu na kumwalika Roho Mtakatifu wa Mungu kuongoza wakati wako pamoja.

## ANGALIA NYUMA

**(Dakika 5)**

Kabla ya kuanza, chukua muda kutazama nyuma.

Mwishoni mwa kipindi kilichopita, kila mtu katika kikundi chako alipewa changamoto ya kufanya mazoezi uliyojifunza.

Chukua muda mfupi kuona jinsi kundi lako lilivyofanya juma hili.

## MAPITIO

**(dakika 1)**

**Katika kikao hiki, tutasikia na kujadili dhana hii:**

- Mzunguko wa Mafunzo

**Na tutaongeza zana hii kwenye seti yetu ya zana:**

- 3/3 Mkutano wa Kikundi

## SOMA

**(Dakika 5)**

**Mzunguko wa Mafunzo**

Kwenye kikao hiki, tutajifunza kuhusu MFUATANO wa MAFUNDISHO ambayo huwasaidia wanafunzi kutoka kwa machache hadi mengi na kufanya umisheni kuwa harakati.

Je, umewahi kujifunza kuendesha baiskeli? Je, umewahi kufundisha mtu mwingine kuendesha? Ikiwa ni hivyo, basi kuna uwezekano unaelewa MFUATANO WA MAFUNDISHO.

Fikiria yaliyopita – kabla uendeshe baiskeli, Huenda ulimuona mtu akiendesha. Hicho ni KIELELEZO.

**KIELELEZO**, SAIDIA, TAZAMA na ACHA

Kielelezo ni kuonyesha mtu mwingine kama mfano jinsi inavyofanywa. Wakati mtoto anapoona mtu kwa mara ya kwanza akiendesha baiskeli, hapo wanapata wazo. Kielelezo ni vivyo hivyo - - sio eti  ifanywe mara kwa mara, na klwa kawaida inastahili kufanywa mara moja.

Fikiria pale nyuma ulipoendesha baiskeli kwa mara ya kwanza. Je, ulitaka tu kuangalia? Ama ulifurahia kupanda na kujaribu? Na je, ikiwa hukupewa fursa na mtu kuendesha?

Kielelezo kingi kinaweza kuumiza mchakato. Kielelezo ni kuonyesha mtu kiasi kidogo tu – na kisha wajaribu. Ni kitu gani kilitendeka ulipojaribu mara ya kwanza? Je, walikupa tu baiskeli na wakaenda zao?

Pengine sivyo. Wakati watu wanajifunza kuendesha baiskeli, mtu huwanaye pale anapoanza kukanyaga. Akitembea kando kukusaidia kuinyosha.

Hiyo ni  KUSAIDIA. KIELELEZO, **SAIDIA**, ANGALIA na ACHA

Kusaidia ni kumsaidia mwanafunzi kuzoesha ujuzi wake lakini hakikisha asianguke kwa nguvu. Kusaidia kunachukua muda mwingi kuliko kielelezo. Lakini sio kwa muda mrefu. Inahitaji kushikiliwa, kuelekezwa na kufundishwa, lakini ni kama kupitia pitia tu vya kimsingi. Sio kumsaidia hadi ukamilifu. Ni kuwasaidia kukanyaga.

Je, unaweza kufikia wakati mtu alikuwa anakimbia kando yako ulipoanza kukanyaga mara ya kwanza na kisha ukaongeza mwendo? Hawangelifanya hivyo kwa muda mrefu, na hungeliweza kuendesha bila kuyumba yumba.

KUSAIDIA ni kumfanya mtu kuenda na kumruhusu aende peke yake. Na anapoanza kuenda, wanakua kielelezo kwa mwanafunzi mwingine ajaye. Hata ikiwa hakuna aliyeshikilia baiskeli, haimaanishi kwamba uko peke yako. Kwa kawaida mtu mwingine huwa anakuangalia – lakini kwa umbali.

Hiyo ni  KUTAZAMA. KIELELEZO, SAIDIA, **ANGALIA** na ACHA

Kutazama ni kumshawishi mwanafunzi hadi awe na ujuzi wake mwenyewe, hiyo yote hufanyika bila kumsaidia kuithibiti. Kuendesha baiskeli, mtu anaweza kuipanda na kuenda kwa haraka, lakini hiyo haimaanishi kwamba anaelewa sheria zote za barabarani.

Kuangalia mtu ni kuhakikisha yuko salama – hata kama hakuna mtu. Kuangalia ni kuhakikisha sio tu kwamba yule mtu anaelewa cha kufanya, na pia aifanye – hata ingawa hakuna mtu anayemwangalia.

Kwenye awamu hii ya Mfuatano wa Mafundisho, mwanafunzi atakua na akiwafundisha wengine jinsi ya kukua … kwa hivyo wafundishe wengine jinsi ya kukua.

Wanafunzi ambao wanaofanya wanafunzi  wanaofanya wanafunzi  wanaofanya wanafunzi. Vivyo hivyo hadi kizazi cha tatu na cha nne.

KUANGALIA ni kuhakikisha kwamba mwanafunzi anakua na sio tu kuwa nia bali pia kusaidia wengine. Kuangalia huchukua muda. Inaweza kuwa mara kumi ili mradi tu Kielelezo na Kusaidia, vikiwekwa pamoja. Inaweza kuwa muda mrefu. Lakini kusubiri kunafaa. Hatimaye - - mwendeshaji ataendesha tu baiskeli.

Hiyo ndio KUACHA kila kitu. KIELELEZO, KUSAIDIA, KUANGALI na **KUACHA**.

Kuacha ni kuhusu kumpa mtu umpendaye zawadi ya mwiasho-zawadi ya uhuru kuacha ni kuhusua kuandaa mtu kuenda sehemu ambayo tayari umekwisha enda lakini pia kuwapa nguvu za kuenda sehemu ambazo

hawajaenda kielezo, kusaidia, kutazama na kuacha mafundisho ya mzunguko.

Kutoka kwa mmoja hadi wengi kutoka sehemu hadi kwa harakati.

## JADILI

**(dakika 10)**

- Je, umewahi kuwa sehemu Mfuatano wa Mafundisho?
- Je, ulifundisha nani au nani alikufundisha?
- Je, mtu yuleyule anaweza kuwa sehemu tofauti za Mzunguko wa Mafunzo huku akijifunza ujuzi tofauti?
- Itakuaje kufundisha mtu kama huyo?

## SHUGHULI

**(Dakika 60 - 90)**

**3/3 Mkutano wa Kikundi**

- ANGALIA NYUMA - Tumia Tii, Treni na Shiriki changamoto za kipindi kilichopita ili kuingia pamoja. (dakika 30)
- TAZAMA JUU - Tumia Marko 5:1-20 kama kifungu cha kusoma cha kikundi chako na ujibu maswali 1-4 katika sehemu ya Angalia. (dakika 30)
- TAZAMA KWA MBELE - Tumia swali la 5, 6, na 7 katika sehemu ya Tazama Mbele ili kukuza jinsi utakavyotii, Kufunza na Kushiriki. (dakika 30)

**Maudhui:**
**KUANGALIA NYUMA**
**Hatua ya 1 - Kutoa Shukrani**

Chukua muda kuwa na kila mtu kushiriki kitu anachoshukuru.

**Hatua ya 2 - Kushiriki Mapambano yako na Kuombeana**

Acha kila mtu katika kikundi chako ashiriki kwa ufupi kitu anachopambana nacho. Acha mtu mwingine awaombee kuhusu kile wanachoshiriki.

**Hatua ya 3 - Kuzingatia Kikundi**

Chukua muda na ukumbuke kwa nini mko pamoja - kumpenda Mungu, kupenda wengine, kushiriki Yesu, na kuwasaidia wengine kumshiriki Yeye pia.

**Hatua ya 4 - Kuingia**

Acha kila mtu ajibu maswali yafuatayo:

- Je, umetii vipi yale ambayo umejifunza hadi sasa?
- Je, umemfundisha nani katika yale uliyojifunza?
- Je! umeshiriki na nani hadithi yako au hadithi ya Mungu tangu tuwe pamoja kama kikundi?)

**KUTAZAMA JUU**
**Hatua ya 1 - Alika Roho Mtakatifu wa Mungu Kuongoza**

Chukua muda kidogo kuomba. Zungumza na Mungu kwa urahisi na kwa ufupi. Mwombe Roho wake Mtakatifu akufundishe kutoka katika kifungu ambacho unakaribia kusoma.

**Hatua ya 2 - Soma Neno la Mungu na Uulize Maswali**

Acha mtu fulani katika kikundi asome kutoka katika Biblia. Unapomaliza kusoma, kikundi kijibu maswali haya mawili:

- Umependa nini kuhusu kifungu hiki?
- Ni jambo gani umepata kuwa gumu au gumu kuelewa?

Soma kifungu kile kile kwa mara ya pili, na kisha kikundi kijibu maswali haya mawili:

- Je, tunaweza kujifunza nini kuhusu watu kutokana na kifungu hiki?
- Tunaweza kujifunza nini kuhusu Mungu kutokana na kifungu hiki?

Kumbuka kushikamana na kifungu na iwe rahisi!

**KUTARAJIA**
**Hatua ya 1 - Kuombea Kusudi la Mungu**

Acha kila mtu katika kikundi chako aombe kimya na muulize Mungu maswali haya:

- Mungu, ninawezaje kutii na kutumia yale unayonifundisha?
- Ni nani ninaweza kufunza kutoka kwa kifungu hiki ili waweze kujifunza kutii na kukupenda Wewe zaidi?
- Je, ungependa nishiriki ushuhuda wangu au Habari zako Njema za Yesu na nani?

Mwombe Roho Mtakatifu wa Mungu akupe majibu mahususi, majina mahususi, na hatua mahususi unazoweza kuchukua kati ya sasa na kundi lako litakapokutana tena.

**Hatua ya 2 - Kukusanya Ahadi**

Uliza kila mtu katika kikundi chako kushiriki kile alichosikia kutoka kwa Bwana kwa kila swali. Mtu anaweza kuwa hajasikia chochote kutoka kwa Bwana kwa swali moja, mbili, au hata zote tatu. Wanaweza tu kuripoti kwamba hawakusikia.

Lakini kumbuka, kundi linapaswa kusikia kutoka kwa Bwana. Yesu alisema, "Kondoo wangu huisikia sauti yangu." Na jinsi hatua zako za utii zinavyokuwa maalum zaidi, ndivyo itakavyokuwa rahisi kuzitii kabla hatujakutana tena.

**Hatua ya 3 - Kutekeleza Mpango wako**

Kabla ya kumaliza muda wako pamoja, fanya Kikundi chako cha 3/3 kigawanywe katika vikundi vidogo vya watu wawili au watatu na fanya kile ambacho umesikia Bwana akikuuliza ufanye.

## JADILI

**(dakika 10)**

- Upenda nini hasa kuhusu kundi la 3/3? Kwa nini?
- Changamoto ilikuwa nini? kwa nini?

## ANGALIA

**(dakika 1)**

**Dhana iliyosikika katika kikao hiki:**

- Mzunguko wa Mafunzo

**Chombo kilisikika katika kikao hiki:**

- 3/3 Mkutano wa Kikundi

**HATUA IFUATAYO**

**TII**

Chagua ujuzi au dhana moja ambayo umejifunza huko Zúme na mshauri mtu ili kuirejesha hadi kizazi cha nne.

**SHIRIKISHA**

Changamoto kwa mtu uliyemshauri kuendelea na mchakato hadi kizazi cha ziada (cha tano).

ZÚME

KIKAO CHA 8

## INGIA

**(dakika 1)**

Waruhusu washiriki wote na mwezeshaji waingie.

Au zume.training/checkin na utumie msimbo: **9870**

## OMBA

**(Dakika 5)**

Omba na kumshukuru Mungu kwa kuwapa kundi lako nguvu, umakini na uaminifu kufika mbali katika mafunzo haya. Mwambie Mungu awe na Roho wake Mtakatifu awakumbushe kila mtu katika kundi kwamba hawezi kufanya lolote bila yeye!

## ANGALIA

Kabla ya kuanza, chukua muda kutazama nyuma.

## NYUMA

**(Dakika 5)**

Mwishoni mwa kipindi kilichopita, kila mtu katika kikundi chako alipewa changamoto ya kufanya mazoezi uliyojifunza.

Chukua muda mfupi kuona jinsi kundi lako lilivyofanya juma hili.

## MAPITIO

**(dakika 1)**

**Katika kikao hiki, tutasikia na kujadili dhana hii:**

- Seli za Uongozi

**Na tutafanya mazoezi ya zana hii kutoka kwa zana yetu ya zana:**

- 3/3 Mkutano wa Kikundi

## SOMA

**(Dakika 5)**

**Seli za Uongozi**

Katika kikao hiki, tutajifunza jinsi CHEMBECHEMBE ZA UONGOZI nhuwatayarisha wafuasi kwa muda mfupi kuwa viongozi wa maisha.

Moja huwa mbili. Mbili huwa nne. Nne huwa nane. Kujizidisha moja moja. Kuongeza vizazi. Ukuaji wa kilelezo.

Huu ndio mfano Mungu aliujenga katika uumbaji wake. Hii ndio njia Mungu ananuia jamaa yake kukua. Tayari tumejifunza kuhusu mfano wa theluthi 3/3 ambao huwabaidilisha watumiaji kuwa wazalishaji, wanafunzi kwa viongozi na wanafunzi kuwa wanaowafanya- wanafunzi.

Angalia Nyuma – Angalia Juu – Angalia Mbele. Jifunze – Tii – Shirikiana.

Hii njia ya kukutana pamoja hufanya ukuaji wa kiroho unaoendelea kwa kila mmoja wa waumini na ukuaji wa uzalishaji katika kundi la wafuasi wa Yesu linaloendelea. Mfano huu huwasaidia wanafunzi kujizidisha.

Itakuaje ikiwa kundi litakuwa pamoja kwa kipindi kifupi tu, Je, bado wataweza kukua na kuzalisha Ufalme wa Mungu? Chembechembe za uongozi ni mfano wa theluthi 3/3 kazini wakati umeelewa kwamba kuna kikomo kwa wakati ambapo kundi linastahili kuwa pamoja.

Chembechembe za uongozi huandaa kila muumini kwa muda mfupi kujifunza mfano wa uzalishaji unaodumu maisha yote. Chembechembe za uongozi huwasaidia wanafunzi kuwa viongozi ambao wataanzisha makundi mapya, kufundisha makanisa mapya, na kuanzisha Chembechembe za uongozi ili kukuza jamaa ya Mungu.

Chembechembe za uongozi hufanya kazi vyema wakati kundi linasonga.

Watu wa kuhamahama, wanafunzi, wanajeshi, wafanya kazi wa ki msimu ambao wanamfuata Yesu hufanya kazi nzuri katika Chembechembe ya uongozi. Kwa sababu ya utamaduni wao, taaluma na msimu wao katika maisha – huenda wanaweza kuwa na wakati mgumu kuanzisha kundi linaloendelea, lakini wanaweza kufundishwa jinsi ya kuanzisha makundi kila mahali waendapo.

Chembechembe za uongozi pia hufanya kazi vyema wakati kundi la watu wanakuwa na imani kwa wakati moja. Jamaa, marafiki, au hata kijiji dogo chaweza kufundishwa kwa muda mfupi kuwa wazalishaji kimaisha – hata bila kufuata mtu binafsi au kufundishwa kiroho. Katika kikao cha awali, tulijifunza na kujizoesha sehemu ya mwisho ya mfano ya theluthi 3/3. Sasa tutajizoesha kwa mfano wote – sehemu zote tatu - - Angalia nyuma, angalia juu, angalia mbele.

## JADILI

**(dakika 10)**

- Je, kuna kundi la wafuasi wa Yesu unaowajua ambao tayari wanakutana au watakuwa tayari kukutana na kuunda Kiini cha Uongozi ili kujifunza Mafunzo ya Zume?
- Ni kitu gani kinahitajika kuwaleta pamoja?

## SHUGHULI

**(Dakika 60 - 90)**

**3/3 Mkutano wa Kikundi**

- ANGALIA NYUMA - Tumia Tii, Treni na Shiriki changamoto za kipindi kilichopita ili kuingia pamoja. (dakika 30)
- TAZAMA JUU - Tumia Matendo 2:42-47 kama kifungu cha kusoma cha kikundi chako na ujibu maswali 1- 4. (Dak 30)
- TAZAMA KWA MBELE - Tumia maswali ya 5, 6, na 7 kukuza jinsi utakavyotii, Kufunza na Kushiriki. (dakika 30)

**Maudhui:**
**KUANGALIA NYUMA**
**Hatua ya 1 - Kutoa Shukrani**

Chukua muda kuwa na kila mtu kushiriki kitu anachoshukuru.

**Hatua ya 2 - Kushiriki Mapambano yako na Kuombeana**

Acha kila mtu katika kikundi chako ashiriki kwa ufupi kitu anachopambana nacho. Acha mtu mwingine awaombee kuhusu kile wanachoshiriki.

**Hatua ya 3 - Kuzingatia Kikundi**

Chukua muda na ukumbuke kwa nini mko pamoja - kumpenda Mungu, kupenda wengine, kushiriki Yesu, na kuwasaidia wengine kumshiriki Yeye pia.

**Hatua ya 4 - Kuingia**

Acha kila mtu ajibu maswali yafuatayo:

- Je, umetii vipi yale ambayo umejifunza hadi sasa?
- Je, umemfundisha nani katika yale uliyojifunza?
- Je! umeshiriki na nani hadithi yako au hadithi ya Mungu tangu tuwe pamoja kama kikundi?)

**KUTAZAMA JUU**

**Hatua ya 1 - Alika Roho Mtakatifu wa Mungu Kuongoza**

Chukua muda kidogo kuomba. Zungumza na Mungu kwa urahisi na kwa ufupi. Mwombe Roho wake Mtakatifu akufundishe kutoka katika kifungu ambacho unakaribia kusoma.

**Hatua ya 2 - Soma Neno la Mungu na Uulize Maswali**

Acha mtu fulani katika kikundi asome kutoka katika Biblia. Unapomaliza kusoma, kikundi kijibu maswali haya mawili:

- Umependa nini kuhusu kifungu hiki?
- Ni jambo gani umepata kuwa gumu au gumu kuelewa?

Soma kifungu kile kile kwa mara ya pili, na kisha kikundi kijibu maswali haya mawili:

- Je, tunaweza kujifunza nini kuhusu watu kutokana na kifungu hiki?
- Tunaweza kujifunza nini kuhusu Mungu kutokana na kifungu hiki?

Kumbuka kushikamana na kifungu na iwe rahisi!

**KUTARAJIA**

**Hatua ya 1 - Kuombea Kusudi la Mungu**

Acha kila mtu katika kikundi chako aombe kimya na muulize Mungu maswali haya:

- Mungu, ninawezaje kutii na kutumia yale unayonifundisha?

- Ni nani ninaweza kufunza kutoka kwa kifungu hiki ili waweze kujifunza kutii na kukupenda Wewe zaidi?
- Je, ungependa nishiriki ushuhuda wangu au Habari zako Njema za Yesu na nani?

Mwombe Roho Mtakatifu wa Mungu akupe majibu mahususi, majina mahususi, na hatua mahususi unazoweza kuchukua kati ya sasa na kundi lako litakapokutana tena.

**Hatua ya 2 - Kukusanya Ahadi**

Uliza kila mtu katika kikundi chako kushiriki kile alichosikia kutoka kwa Bwana kwa kila swali. Mtu anaweza kuwa hajasikia chochote kutoka kwa Bwana kwa swali moja, mbili, au hata zote tatu. Wanaweza tu kuripoti kwamba hawakusikia.

Lakini kumbuka, kundi linapaswa kusikia kutoka kwa Bwana. Yesu alisema, “Kondoo wangu huisikia sauti yangu.” Na jinsi hatua zako za utii zinavyokuwa maalum zaidi, ndivyo itakavyokuwa rahisi kuzitii kabla hatujakutana tena.

**Hatua ya 3 - Kutekeleza Mpango wako**

Kabla ya kumaliza muda wako pamoja, fanya Kikundi chako cha 3/3 kigawanywe katika vikundi vidogo vya watu wawili au watatu na fanya kile ambacho umesikia Bwana akikuuliza ufanye.

## ANGALIA

**(dakika 1)**

**Dhana kutoka kwa kipindi hiki:**

- Seli za Uongozi

**Zana kutoka kwa kipindi hiki:**

- 3/3 Mkutano wa Kikundi

**HATUA IFUATAYO**

**TII**

Chagua baadhi ya watu kutoka kwenye Orodha yako ya 100 ambao tayari ni waumini. Waelezee Seli za Uongozi na uone kama watavutiwa kuwa sehemu ya moja.

**SHIRIKISHA**

Omba na umuulize Mungu ambaye anataka ushiriki naye zana ya Kiini cha Uongozi kabla ya kikundi chako kukutana tena. Changamoto waishiriki na mtu mwingine.

# KIKAO CHA 9

## INGIA

**(dakika 1)**

Waruhusu washiriki wote na mwezeshaji waingie.

Au zume.training/checkin na utumie msimbo: **1355**

## OMBA

**(Dakika 5)**

